# UHALISIAJABU UNAVYOJITOKEZA KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* NA *UTENZI WA FUMO LIYONGO*

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
EAST AFRICANA

NA

ONCHWATI S. JARED

**TASNIFU HII IMEWASILILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KISWAHILI**

**KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

1600279
University of Nairobi Library Thesis
2016

**IDARA YA LUGHA NA ISIMU.**

**NOVEMBA, 2016**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kingine.

______________________ 10/10/2016 ______________________

Sahihi

**Jared Shitandah Onchwati** **Tarehe**
**(Mtahiniwa)**

**NAMBARI YA USAJILI C50/67041/2013**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

______________________ 8/11/16 ______________________

**Prof. Kineene wa Mutiso** **Tarehe**

**(Msimamizi)**

______________________ 11/10/2016 ______________________

**Prof. Rayya Timammy** **Tarehe**

**(Msimamizi)**

# IKISIRI

Utafiti huu ulikusudia kuonyesha sifa za kiuhalisiajabu kama zinavyojitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tulifanyanya hivyo kwa kuwarejelea baadhi ya wahusika na mandhari kama yalivyosawiriwa katika tenzi zenyewe. Madhumuni yetu katika utafiti huu yalikuwa kudhihirisha uhalisiajabu ulivyosawiriwa katika tenzi. Aidha tulibaini kuwa sifa za kiuhalisiajabu zilikuwa nguzo muhimu kwa watunzi wa tenzi hizi katika kufikia malengo yao mbali na wao kutengana kiwakati na kiumri.

Tuliufikia uchanganuzi huu baada ya kutambua kuwa, uhalisiajabu katika tenzi haujatafitiwa sana ilihali ni mojawapo ya fasihi kongwe zaidi kuliko riwaya na tamthilia. Tumeangalia sifa za takribani wahusika wote katika tenzi hizi, mazingira walimolelewa pamoja na jamii zilizowazaa na kuwalea. Vile vile tumeangalia umuhimu wao katika jamii zao. Data ilikusanywa maktabani, mtandaoni na kuchanganuliwa kwa misingi ya nadharia ya uhalisiajabu iliyoasisiwa na Franz Roh (1925).

Matokeo ya utafiti wetu yalilingana na nadharia tete zilizoongoza mchakato mzima wa utafiti wetu. Kupitia kwa sifa za wahusika na za mandhari tuligundua kuwa tenzi zimesheheni uhalisiajabu sawia na vipera vingine vya fasihi. Mbali na tenzi zote mbili kudhihirisha sifa za kiuhalisiajabu, ilidhihirika kuwa dhamira za watunzi wa tenzi hizi zimetofautiana mno. Tuligundua kuwa uhalisiajabu husawiriwa vyema katika mandhari, wahusika wenye sifa za kibinadamu na wale wasiokuwa na sifa za kibinadamu. Aidha tulibaini kuwa wahusika wa aina hizi zote, ni sehemu muhimu katika kujenga historia ya jamii zao na dunia yote kwa ujumla.

## TABARUKU

Tasnifu hii namtabarukia mamangu mzazi Bi.Marcella Anyega aliyenifunza maana ya bidii, ukweli, unyenyekevu, wema na upole maishani. Mungu amshehenezee maisha na afya njema daima.

Pia ninamtabarukia mamangu mkubwa Bi. Pacificah Anyega, Babangu mpendwa Bw. Paul Onchwati Ayiema, Marehemu nyanyangu Bonareri, Babu Anyega Nyang'eni na Mogeni walionifunza kutambaa kimasomo maishani. Ndugu yangu Monda Josephat, Nyangeri Vincent, Okeri Wilson, dada Moraa Linet, Mary Tanui, Nyaboke Jackline na Vane Bonareri kwa kunimotisha na kunipa msaada usio kifani kila wakati nilipopungukiwa. Baraka zake Allah ziwaandame daima dawamu.

Aidha, sitamsahau mke wangu Annah Kerubo na mwanangu Loice Bonareri kwa kunivumilia muda wote ambao sikushirikiana nao kwa mambo mengi kila mara waliponihitaji. Ninawasafia nia wote watambue dhima ya elimu katika maisha ya dunia hii yenye utata na matata chungu nzima. Heri na ije kwenu nyote.

## SHUKRANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema nilipokuwa ninatafuta maarifa. Pasipo yeye ningegeuka mifupa mikavu. Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu: Prof. Kineene wa Mutiso na Prof. Rayya Timammy kwa kunipa mwelekeo usio kipimo tangu mwanzo hadi tamati. Ninatoa shukrani kwao kwani waliniongoza kwa njia za kiusomi ambazo ni za kipekee. Baraka nyingi ziwafikie popote walipo.

Aidha ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu katika idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi kwa kuniandaa kiakademia hadi kuweza kukabili kazi za kitaalamu: Mwenyekiti wa idara Prof. Iribe Mwangi, Prof. John Habwe, Dkt, Mwenda Mbatiah, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mbuthia Evans, Dkt. Swaleh Amiri na Mwalimu Mungania B. Ninawaombea Mungu awashehenezee neema. Isitoshe ninawashukuru mashekhe na watumishi wa Mungu walioshirikiana nami bega kwa bega katika kutatua changamoto nyingi zilizonikumba. Pia shukrani jazila ziwaendee wanafunzi wa uzamili wenzangu tulioshirikiana kwa hali na mali. Kwa kweli msingalikuwepo nisingalifika umbali huu: Mogusu, Wadhe, Nyamari, Chesebe, Bosibori, Asha, Kimetto, Zahara, na wengine. Nimeshukuru kwa kuwajua, mbali na kushirikiana masomoni. Hatimaye niwashukuru marafiki zangu walionitia moyo wa kuendelea kutambaa kimasomo hata kama ni kwa kuuma meno. Shukrani kwenu nyote.

# YALIYOMO

**UNGAMO** .......... ii
**TABARUKU** .......... iii
**SHUKRANI** .......... iv
**IKISIRI** .......... v
**YALIYOMO** .......... vi

**SURA YA KWANZA**

1.0 Utangulizi .......... 1
1.1 Tatizo la utafiti .......... 2
1.2 Malengo ya utafiti .......... 3
1.3 Nadharia tete .......... 4
1.4 Sababu za kuchagua mada .......... 4
1.5 Upeo na mipaka. .......... 4
1.6 Msingi wa nadharia .......... 5
1.7 Mihimili ya nadharia .......... 7
1.8 Mapitio ya vitabu .......... 8
1.9 Mbinu za utafiti .......... 11

**SURA YA PILI**

**HISTORIA YA TENZI NA MATUKIO YA KIAJABU KATIKA *UTENZI WA FUMO LIYONGO* NA *UKAWAFI WA MIIRAJI.***

2.0 Utangulizi .......... 12
2.1 Historia ya tendi .......... 12
2.2 Historia ya Waswahili. .......... 15
2.3 Mazoea ya waandishi wa tenzi. .......... 17
2.4 Kisa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* .......... 17
2.5 Usuli wa Mtume Kabla ya Miiraji .......... 20
2.6 Kisa cha Miiraji. .......... 22
2.7 Dhamira katika *Ukawafi wa Miiraji.* .......... 26

**SURA YA TATU**

**KUBAINISHA SIFA ZA WAHUSIKA NA MANDHARI KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* NA *UTENZI WA FUMO LIYONGO***

3.0 Utangulizi .......... 29
3.1 Wahusika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* .......... 31

3.1.1 Sifa za Fumo Liyongo. .... 32
3.2 Sifa za wahusika katika *Ukawafi wa Miiraji* .... 35
3.2.1 Sifa za Allah .... 36
3.2.2 Sifa za mtume Muhammad .... 37
3.2.3 Sifa za walinzi / mitume wa mbingu saba .... 39
3.2.4 Sifa za malaika. .... 40
3.2.5 Sifa za mke mwema .... 40
3.2.6 Sifa za watu waovu .... 41
3.2.7 Sifa za buraki .... 41
3.3 Sifa za Mandhari .... 42
3.3.1 Mandhari ya kisimani .... 42
3.3.2 Mandhari ya mbinguni .... 43
3.3.3 Mandhari ya jahanamu .... 43

**SURA YA NNE**

**SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA *UTENZI WA FUMO LIYONGO* NA *UKAWAFI WA MIIRAJI***

4.0 Utangulizi .... 45
4.1 Matukio yanayoogofya na yanayoshangaza katika Utenzi wa Fumo Liyongo. .... 45
4.2 Matukio ambayo yanaogofya na kushangaza katika *Ukawafi wa Miiraji.* .... 48
4.3 Mandhari ambayo yanaaogofya na kushangaza .... 50
4.4 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* .... 50
4.5 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali katika *Ukawafi wa Miiraji* .... 51
4.6 Matukio ya kifantasia katika *Utenzi wa Miiraji.* .... 52
4.7 Matukio ya kifantasia katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.* .... 53
4.8 Wakati hausongi katika kazi ya uhalisiajabu .... 54
4.9 Upanuaji wa mwanda wa kisimulizi .... 55

**SURA YA TANO**

**UMUHIMU WA SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* NA *UTENZI WA FUMO LIYONGO***

5.0 Utangulizi. .... 57
5.1 Fahari kwa wanajamii na waumini wa dini. .... 57
5.2 Kitambulisho cha kidini na kijamii. .... 59
5.3 Ukombozi, uzalendo na undugu baina ya wanajamii. .... 60

5.4 Kuimarishwa kwa dini ya kiislamu. ........ 61

5.5 Kielelezo mfano cha kuigwa. ........ 62

5.6 Historia ya jamii husika. ........ 63

## SURA YA SITA

6.0 Mahitimisho ........ 65

**6.2 MAREJELEO ........ 69**

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Chunguzi nyingi zimefanywa na wataalamu zinazohusu ushairi hasa tendi mbalimbali. Baadhi ya tafiti hizi zimefanywa kwa kuangazia, maudhui, sifa za wahusika, dhamira, mazingira, fani, tamathali za usemi, mahusiano kati ya dini na lugha ya Kiswahili na mengine mengi. Kuna tafiti zilizowahi kuchapishwa ambazo zimesheheni mambo na matukio ya kiajabu au ya kushangaza yanayoakisi kweli fulani maishani. Hisia zetu zimevutiwa katika kutafitia uhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

*Utenzi wa Fumo Liyongo* ulitungwa naye Muhammad Kijumwa (Muhammad bin Umar al-Bakry) mnamo mwaka 1331 Hijriya (1913). Utenzi huu unamhusu shujaa Fumo Liyongo wa Bauri ambaye aliishi katika karne ya kumi na tatu Masihiya. Mtunzi amesimulia maisha ya shujaa huyu kwa njia ya kishairi. Japo kuna utata kuhusu tarehe kamili aliyozaliwa Liyongo, tarehe inayoelekea kukubalika zaidi ni ile ya karne ya 13 hadi 14 kulingana na kitabu cha Tarehe ya Pate. Kwa mujibu wautangulizi katika utenzi wenyewe Chiraghdin (1977), miongoni mwa mabingwa wengine anaeleza tarehe kamili aliyowahi kuishi shujaa huyu ambayo ni 555-600 Hijriya, miaka inayoafikiana na 1160-1204 Masihiya. Mtunzi anatueleza kuwa Liyongo aliishi pwani ya kaskazini mwa Kenya kwenye maeneo ya Ozi na Pate mnamo karne ya 14 au kabla. Mamake aliitwa Samoe Mwana. Alikuwa shujaa, manju wa ngoma, malenga, na mwindaji hodari. Kwa upande wa dini, hakuna uhakika kama alikuwa mwislamu au mkristu japo nyimbo zake zinaonyesha kuwa huenda alikuwa mfuasi wa dini ya jadi ya Waswahili. Liyongo alikuwa akiwinda na kufanya biashara sehemu za bara karibu na Pate. Mtunzi, yuwasimulia tangu Liyongo alivoinukia kuwa na nguvu nyingi zaidi kuliko za mwanadamu wa kawaida. Mwandishi anafafanua umbo lake lilivyokuwa nene, namna alivyopendeza kwa watu wengi hata Wagalla wakamtaka aowe msichana wa kabila lao. Sifa hizi zilipelekea Liyongo kuenziwa na watu wengi, jambo lililosababisha Mfalme wa Pate kujawa na fitina hata akatafuta kila hila ili amuue Liyongo. Hatimaye mfalme alimshawishi mtoto wa Liyongo kutimiza haja yake hiyo baada ya mbinu zake mbili kushindwa. Liyongo aliweka makazi yake Ozi na alifia na kuzikwa Kipini, mahali paitwapo Ungwana wa Mashaha.

Mtunzi wa mwanzo kabisa wa *Ukawafi wa Miiraji* ni Najmu'd al-Ghaitty kama inavyodokezwa na utenzi wenyewe katika dibaji. Utenzi huu ulitungwa kwa lugha ya Kiarabu, baadaye ulitafsiriwa katika Lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha zingine nyingi ulimwenguni. Baadaye mashehe wengi walitunga tenzi nyingi za *Miiraji* ambazo zinatofautiana katika vipengele mbalimbali kutoka kwa mtunzi mmoja hadi mwingine. Kwa mujibu wa Mutiso (2016), hadi hii leo bado tenzi zingine za *Miiraji* zingali zinatungwa. Tenzi hizi zinatofautiana kwa yaliyomo kwani kuna matukio yaliyodondoshwa katika utendi mmoja ilihali kwa mwingine matukio fulani yamechopekwa. Katika utafiti wetu, tumeangazia *Ukawafi wa Miiraji* ulioandikwa naye Shehe Al-'Amin bin Aly (beti za 112). Utenzi huu unahusu matukio yanayoaminika kuwa ya kweli wakati Mtume alipopaa kwenda mbinguni na aliporejea kuwaeleza Makureishi yote aliyoonyeshwa. Safari inaanza pale ambapo malaika Jiburili, Mikaili na malaika mwingine, wanambeba mtume Muhammad, kisha wanamlaza. Malaika Jiburili anafungua kifua cha Muhammad ili kukitakasa. Anakiosha mara tatu anatoa uchafu uliokuwa ndani. Kisha anaweka ndaniye kitu cha dhamana safi, chenye hekima na imani. Baadaye anamshona na kumtia mhuri wa utume. Mtume anapandishwa juu ya mnyama anayeitwa buraki, kisha anatembezwa huku akionyeshwa matukio mbalimbali na maana zake kufasiriwa. Hatimaye wanafika katika nyumba takatifu ambapo buraki anafungwa ukutani. Mtume anapozidiwa na kiu, anapewa maziwa, asali na pombe. Yeye anachagua kunywa maziwa. baadaye Miiraji inashuka kutoka mbinguni ambayo Mtume anapandia kuelekea mbinguni. Mtume anaelezwa mengi huku akionyeshwa milango ya mbingu ya kwanza hadi ya saba. Kwa kila mbingu Mtume anakutana na mitume wengine kama Adam, Isa, Yahya, Yusufu mwana wa Yakubu, Idirisi, Haruni, Musa na Ibrahim. Mwishowe anakutana na Mungu ambaye anampa sala hamsini ambazo zinapunguzwa hadi tano kwa siku.

## 1.1 Tatizo la utafiti

Wataalamu mbalimbali wametoa fafanuzi kuhusu uhalisiajabu. Hawa ni kama vile Breton (1969) anayetoa mawazo mawili tofauti yanayoelekea kufanana anaposema kwamba, matumizi ya mbinu, kama vile maandishi ya kufikirika, mawazo ya vitu vilivyo na visivyo kweli afikiriayo mtu na michezo ya maneno inayovutia mno kiasi cha kufanya yaliyomo akilini kudhihirika.

Pia anaeleza uhalisiajabu kuwa ni kubainisha mtazamo wa hali halisi wa wanauhalisiajabu na kueleza matakwa ya kifikra kupitia kwa mtazamo wa hali ya ndoto na uhuru wa mawazo. Wasomi wengine wanatoa mawazo yanayoelekea kufanana na haya ya Breton. Lois Parkinson, Zamora, Wendy B. na Faris (1995:27), wanatoa rai kwamba "Uhalisiajabu unaafiki kuutalii-na kukaidi-mipaka, si hoja kama mipaka hiyo ni ya kiontolojia, ya kisiasa, kijiografia au kiutanzu" Zamora na Faris (1995:5) kwa kuyazingatia mawazo ya wataalamu hawa, tumechunguza jinsi uhalisiajabu unavyodhihirika katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tumeonyesha ni kwa nini uhalisiajabu ni njia nzuri ya kusoma na kuzielewa tenzi hizi mbili. Tatizo hili ni muhimu kushughulikiwa kwa vile watunzi wa tenzi hizi wametumia lugha ya mkato, uhusika usiozoeleka na mandhari ya kustaajabisha katika kuzitunga kazi zao. Waandishi hawa wameusawiri uhalisiajabu katika kuwakweza baadhi ya wahusika na wakati huo huo kuwatweza wahusika wengine. Utunzi wa sampuli hii unahitaji utafiti wa kina kirefu ili kuweka wazi sifa za kazi ya watunzi hawa. Kuna mwachano mkubwa kati ya mambo ya kweli katika dunia halisi na ya kindotoni. Tumedhamiria kuchunguza uhalisiajabu katika kitengo cha wahusika na uhusika pamoja na madhari ya matukio katika tenzi hizi.

## 1.2 Malengo ya utafiti

a) Kufafanua matukio ya kiuhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

b) Kuchunguza jinsi sifa za kiuhalisiajabu zinavyojitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

c) Kutathimini mtazamo wa waandishi hawa kuhusu swala la uhalisiajabu unavyodhihirika katika tenzi hizi mbili.

d) Kulinganisha sifa za wahusika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi* wa *Miiraji.*

## 1.3 Nadharia tete.

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

a) Kuna sifa za uhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

b) Uhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utendi wa Fumo Liyongo* una umuhimu mkubwa katika kuuendeleza ushujaa/dini.

## 1.4 Sababu za kuchagua mada

Tumechagua kutafitia mada hii kwa sababu zifuatazo: Watafiti waliotafitia tenzi hizi, walifanya hivyo kwa mikondo tofauti na yetu. Hii ina maana kwamba uhalisiajabu haujashughulikiwa kwa kuzingatia tenzi hizi. Mbali na tasnifu yake Vutagwa (2013) iliyoangazia *Utenzi wa Fatuma,* watafiti wengi wametafitia uhalisiajabu katika riwaya na tamthilia. Kwa mfano, kuna utafiti uliofanywa na Mwangi (2013) ambao unaangazia riwaya, *Babu alipofufuka* na *Bina-Anadamu.* Mbali na utafiti huu, watafiti wengi wameangazia uhalisiajabu katika aina zingine za fasihi na wakakosa kubaini kuwa tenzi kama kazi zingine za kifasihi zimesheheni uhalisiajabu. Wengi wa watafiti hawaamini kuwa ushairi kama tawi la fasihi andishi unaowasilisha ujumbe wake kwa mkato na wakati huo huo huwasilisha ujumbe sawia na tanzu zingine. Tumegundua kuwa kuna pengo la uhalisiajabu hasa katika tendi kwani wengi wa watafiti wamejikita katika tanzu zingine hasa riwaya. Aidha kuna pengo linalodhihirika katika tenzi zenyewe kwa ujumla. Kutokana na sababu ambazo tumezitaja hapo juu, ndizo zilizotupelekea kuchagua mada hii. Tumebaini, mandhari, matukio ya kiuhalisiajabu na umuhimu wao katika *Utendi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji.*

## 1.5 Upeo na mipaka.

Utafiti huu utajikita katika kushughulikia *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Watunzi wa tenzi hizi wameandika tenzi zingine lakini tenzi hizi mbili zitatoshea kwa mahitaji ya utafiti wetu. Tumejikita katika tenzi hizi kwa sababu tungo hizi zinaelekea kuafiki mwelekeo wetu wa uhalisiajabu. Zipo tungo zingine ambazo zimeandikwa lakini tumechagua tenzi hizi mbili za waandishi wawili tofauti waliotengwa kiwakati, kiumri na kijiografia. Aidha tumechagua tenzi hizi mbili ili

kubaini ikiwa kuna uhusiano wowote mbali na utengano ulio kati yao. Tumetafiti kazi hizi kwa kutumia nadharia ya uhalisiajabu inayohusishwa na Roh (1925) ambaye alikuwa ni mhakiki na mwanzilishi wake. Tenzi hizi mbili zimeshughulikiwa ili kuthibitisha madai yetu ya uhusika, wahusika pamoja na mandhari kwa mwelekeo wa uhalisiajabu.

### 1.6 Msingi wa nadharia

Katika utafiti huu, tumeongozwa na nadharia ya uhalisiajabu/uhalisi mazingaombwe kwani tunaamini itaafiki utafiti wetu. Wamitila (2003:234) anaeleza kuwa, uhalisiajabu ni dhana iliyobuniwa na msanii wa Ujerumani, Roh(1925:88) katika kitabu chake *Nach-expressionismus, magischer Realismus* na inahusishwa na waandishi wa Marekani ya Kusini au hata nchi zinazoitwa ulimwengu wa tatu na hutambulishwa na sifa mbalimbali. Sifa hizi ni za kuyaelezea matukio ya kifantasia, ya kiajabu au kichawi kwa namna ya moja kwa moja na kwa namna inayoyafanya yaonekane kama ya kawaida tu. Roh (1925:45) anasema kuwa, mpaka uliopo kati ya mambo yanayoweza kupatikana katika ulimwengu halisi na yasiyowezekana huwa mdogo sana.

Walibora (2010:143) akimnukuu Abrams (1999) anasema kuwa Istilahi ya uhalisiamazingaombwe ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920, inatumika kufasili kazi bunilizi za kinathari za Jorge Luis Borges wa Argentina, na hali kadhalika kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez (1967) wa Kolombia, Isabel Allende (1982) wa Chile, Gunter Grass (1959) wa Ujerumani, Italo Calvino (1952) wa Italia, na John Fowles (1945) wa Uingereza. Waandishi hawa wanasukanisha uhalisia uliochongwa kwa njia maalum katika ruwaza inayobadilika badilika. Wanawakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina, sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto, na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili na hekaya.

Akielezea uhalisiajabu, Mbatiah (2002:60) anafafanua kuwa istilahi ya uhalisiajabu inatumiwa kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo, mitindo ya uhalisiajabu inaelezwa kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa, ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabu ajabu, hutokana na maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Anasema kuwa uhalisia wa kimaajabu huhusishwa zaidi na nchi zinazoendelea kutoka Bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia.

Kutokana na maelezo ya waandishi hawa, tunaona ya kuwa, wanauhalisiajabu hutumia sifa zinazobainisha kazi zao ingawa wana mitazamo na imani tofauti za kimsingi. Njogu na Wafula (2007:114) wanasema kuwa uhalisiamazingaombwe ni nadharia ambayo inakiuka sifa za uhalisia kama zilivyoelezwa na waandishi wa karne ya kumi na tisa na ishirini. Katika uhalisiajabu, matukio yasiyoaminika (ya kifantasia) husawiriwa. Mambo ya kiajabu yanaelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida. Hali ya kushangaza na kuogofya huwasilishwa kuwa ya kawaida katika uhalisiajabu; ndoto na uhalisi vinachanganywa.

Hoja kwamba Roh ndiye mwasisi wa uhalisiamazingaombwe inapingwa au kurekebishwa na wahakiki kama vile Christopher Warnes anayedai kwamba, matumizi ya awali kabisa ya istilahi ya 'uhalisiamazingaombwe' yanapatikana katika maandishi ya mshairi Fridrich Freiherr von Hardenberg, maarufu kwa lakabu ya kishairi Novalis. Warnes (2006:488) anasema kuwa, Novalis hakuikuza mno dhana ya uhalisiamazingaombwe pamoja na kwamba alikuwa wa kwanza kuitumia. Labda ndio sababu wengi humtaja Roh aliyeitumia kinadharia kauli ya uhalisiamazingaombwe mwaka 1925 kama mwasisi wa istilahi hii. Walibora (2010:146) anasema kuwa, uhalisiamazingaombwe unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama mkabala wa kuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka, kuhujumu au kuvuruga usimulizi mbali na kukaidi kaida za lugha na ingawa ni mkabala wa kifasihi unaonasibishwa zaidi na waandishi wa Amerika Kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za janibu mbalimbali zikizungumzwa kwa dayalojia hii.

## 1.7 Mihimili ya nadharia

Kutokana na kazi za Breton (1924), Zamora (1995), Roh (1925) na William (2003) baadhi ya mihimili ya nadharia ya uhalisi ajabu ni:

Matukio ya kifantasia yanayoonekana ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya au kutisha. Katika uhalisiajabu, hakuna mipaka kati ya uhalisi na ndoto. Pengine mtu anapoota ndipo yu katika hali halisi na vivyo hivyo anapokuwa katika hali halisi ndipo yumo ndotoni.

Mipaka ya kijamii, kitaifa na kimataifa huvunjwa, yaani wanauhalisiajabu wanajadili mambo yanayohusu ulimwengu kwa jumla bila kujiweka katika maeneo fulani finyu kama vile jamii, nchi au bara moja.Wakati na mahali zina uhusiano wa kiduara badala ya kistari. Inamaanisha kwamba jambo linaweza kujirudia kwa sura nyingine mahali pengine. Uhalisiajabu huu pia, umefungamana na sanaajadi kama vile visasili.

Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Mtindo wa baadhi ya tanzu za fasihi simulizi hutumika. Jambo hili hufanywa kwa kumpeleka msomaji kwenye safari ya hali na matukio ya kikweli na yanayowezekana. Aidha, wasanii hutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili.

Mandhari ni sehemu muhimu sana katika aina hii ya fasihi. Wanyama, majitu, misitu mikubwa yenye giza totoro, wanyama hatari na mazimwi hurejelewa. Vile vile, mimea, mito, maziwa na bahari huchukua nafasi muhimu katika uandishi wa uhalisiajabu. Uhalisiajabu huenda kinyume cha mahusiano ya matukio katika maisha ya mja kiutengano. Hali mbalimbali kama vile uhalisi na ndoto, kifo na uhai, usasa na uzamani, shamba na mjini, ugeni na utamaduni huonekana zikiingiliana.

Ni muhimu kutaja kwamba, si mihimili yote ambayo imetumika katika utafiti wetu. Iliyotumika ni ile tu, iliyofaa zaidi kufafanua tenzi tumezichunguza ili kuweka wazi dhana ya uhalisiajabu.

## 1.8 Mapitio ya vitabu

Kazi nyingi tulizozipitia kuhusu somo hili zimejikita katika mashairi ya kale yaliyoandikwa kabla ya karne ya ishirini. Ni katika kipindi hiki tenzi nyingi za kidini zilitungwa. Mbali na hayo zipo tafiti zilizowahi kufanywa zikiangazia tenzi japo tulipata chache ambazo tulipitia. Kwa mfano tasnifu yake Vutagwa (2013), ambayo iliangazia *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Katika tasnifu hii, mtafiti anausawiri uhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kidini. Aidha anaangazia sifa za kiuhalisiajabu pamoja na umuhimu wake. Kazi hii ilitusaidia kuelewa kwa kina matukio ya kushangaza katika tenzi zote mbili kwa sababu mtafiti huyu amebainisha sifa za kiajabu katika *Utenzi wa Mwana Fatuma.* Hata hivyo kazi yake ni tofauti na yetu kwani yeye ameangazia utenzi mmoja tofauti na tenzi mbili tunazotafitia. Isitoshe sisi tumezingatia uhulisiajabu katika uhusika, wahusika pamoja na mandhari kazi ambayo ni tofauti na vile alivyoangazia uhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kidini.

Tumesoma tasnifu ya Mwangi (2013) ambapo ametafitia riwaya mpya *Babu alipofufuka* na *Watu wa Gehenna.* Yeye, ametumia nadharia sawia na yetu: Nadharia ya uhalisiajabu. Mtafiti huyu anaonyesha namna ambavyo mazingira huchangia katika kubainisha sifa za uhusika na wahusika. Mhusika anayeishi katika jumba la kifahari huathirika na mazingira hayo kwa kuwa atavaa mavazi ghali, awe na watumishi wengi, burudani, makasri na mengine mengi. Haya ni tofauti na mhusika anayeishi kibandani. Vivyo hivyo mhusika anayeishi mbinguni, atakuwa na uwezo au sifa za uungu tofauti na anayeishi duniani. Kwa mfano, katika riwaya *Babu Alipofufuka,* mandhari yenye uhalisia yanapatikana mwanzoni mwa riwaya ambapo mhusika K anaishi katika ulimwengu halisi na kisha anaingia katika ulimwengu wa kimawazo, na kurejea tena katika ulimwengu halisi. Mandhari haya yanabadilika vivyo hivyo kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Katika riwaya nzima, uhalisiajabu umetokea mara nyingi kuanzia wakati maisha ya mhusika K yanapoingiliwa na mzuka wa babu yake. Ufafanuzi huu wa wahusika na uhusika kuingiliana na mandhari yao ulitufaa sana katika kuwaelewa wahusika katika tenzi tunazochunguza. Mbali na mandhari mtafiti huyu ameangazia wahusika majagina ambao wana nguvu za kiajabu na hivyo kutambulika kwa urahisi. Utafiti huu ulitufaa sana ikizingatiwa kuwa katika utafiti wetu kuna wahusika wa sampuli hiyo kwa mfano Fumo Liyongo. Aidha matukio yanayotokea katika mandhari ya mbinguni hasa katika riwaya ya

*Watu wa Gehenna* yanafanana mno na matukio katika *Ukawafi wa Miiraji*. Kwa mfano, katika riwaya hii, kuna kuadhibiwa kwa wasiotii sheria za Mungu ilihali watiifu huzawadiwa naye Muumba. Hali kama hii inafanana katika tenzi tunazochunguza hasa *Ukawafi wa Miiraji*. Tofauti na utafiti wetu, tasnifu hii iliangazia uhalisiajabu katika riwaya mpya ilihali sisi tumejikita katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji*.

Katika tamthilia ya *Kifo kisimani* mwandishi Mberia (2002), anausawiri uongozi mbaya kupitia kwa mhusika Bokono Mtemi. Katika mazungumzo ya kitamthilia, washauri wa Bokono wanampotosha kwa kumshauri visivyo. Askari wa kiongozi huyu wanawadhulumu wananchi kwa kuwanyima haki ya kutumia rasilimali za mji wa Cheneo. Maudhui ya ubaguzi, utabaka na ufujaji wa fedha za umma yanachangia kuonyesha sifa za uongozi mbaya. Usaliti ni maudhui ambayo mwandishi huyu ameyakuza vyema kupitia kwa mhusika Gege. Mawazo yetu yalivutiwa sana na maudhui haya kwa sababau ndio yaliyokuwa kiini chetu cha kusoma tamthilia hii. Mhusika Gege Biuki anapewa ahadi chungu nzima ili amuue nduguye-Mwelusi. Mhusika huyo anajibidiisha kwa kila namna hadi anakatisha maisha ya Mwelusi alipokuwa ameenda kisimani. Usaliti huu unambainikia mamake Mwelusi ndotoni, anaota kuona kichwa cha simba kisimani ambacho kinabadilika na kufanana na cha mwanawe-Mwelusi. Usomaji wa Tamthilia hii ulitufaa pakubwa katika kuuelewa *Utenzi wa Fumo Liyongo* kikamilifu. Tuligundua mfanano wa kutajika katika mhusika Mwelusi wa tamthiliani na Fumo Liyongo wa utenzini. Usomaji wetu ulitupelekea kukisia kuwa kwa namna fulani Mberia (2002), huenda alichota malighafi ya utunzi wake kutokana na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Utafiti wetu umechukua mkondo tofauti na kazi hii ya tamthilia kwa kuwa tumechunguza utenzi wenyewe tofauti na majibizano ya kitamthilia. Aidha dhamira yetu imekuwa ya kudhihirisha uhalisiajabu katika tenzi mbili, *Utenzi wa Fumo Liyongo* ukiwemo swala ambalo ni tofauti na uongozi mbaya unaobainishwa tamthiliani.

Katika uhakiki wao wa tamthilia ya *Mashetani*, Njogu na Chimerah (1999:200-201) wanatujulisha kwamba Juma na Kitaru wameamua kucheza mchezo wa shetani na binadamu ili waielewe barabara hali yao ya sasa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa jumla. Katika mchezo huu, kuna mgogoro uliopo baina ya shetani (Juma) na binadamu (Kitaru). Kitaru anafahamikiwa na migogoro, migongano na mikinzano ya

kijamii katika ndoto. Kwa njia ya ndoto, anaifahamu mifumo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii na jinsi inavyomwathiri yeye na jamii nzima. Kutokana na mchezo huu, tuliweza kuelewa ndoto kama mhimili wa uhalisiajabu ambao umetufaa katika utafiti wetu. Aidha kupitia kwa tamthilia hii tuliweza kuelewa zaidi sifa za wahusika ambazo zimejitokeza vyema kupitia migogoro iliyomo katika utenzi hasa *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

Katika tamthilia ya *Amezidi* mwandishi Muhammad (1995) anaonyesha hali moja wajipatao wahusika wawili Ame na Zidi. Wahusika hawa wamo katika hali yenye uhitaji mkubwa miaka mingi baada ya ukoloni. Wahusika hawa wanaishi pangoni lakini wanaliita kasri, wanamiliki sofa lisilokuwepo, wanakalia sofa lisilokuwepo, wana friji na rediogramu ambavyo havipo, wanalalia kitanda na mto usiokuwepo ilihali ni majani. Wanaonyeshana maegesho ya magari ya kifahari ambayo hayapo. Tamthilia hii imetusaidia sana kuelewa sifa za kiuhalisiajabu. Tofauti na tamthilia hii, utafiti wetu tumeangazia tenzi ambazo zinasheheni sifa za uhalisiajabu.

Tumebaini sifa za uhalisiajabu katika hadithi fupi ambazo zimekuwa kijalizo katika mapitio yetu. Kwa mfano katika Wamitila (2004), mhusika Mayai waziri wa maradhi anaona mlango wa nyumba yake ukifunguka kabla hajainuka kitini ili aende kulala. Hakuna chochote kinachotokea katika mlango uliofunguka ila waziri anasikia mishindo ya watu wengi wakipiga makitaimu. Inapofika saa sita usiku, mara hii Waziri anasikia dirisha likigongwa, dirisha linaanza kufunguka polepole. Mwishowe anasikia sauti ya mwanawe (Ukombozi) ikimwita, anapomwita mwanawe, anasikia mishindo ya viatu vya mtoto mdogo ikitembea kwenda shuleni. Mlio ambao alikuwa ameuzoea. Inapofika saa kumi, waziri anaamka na anashangaa kwa kile anachokiona. Anaona watoto tisa, na wa kumi ni Ukombozi ambaye amesimama akiwapakia wenzake jamu na siagi kwenye mkate. Anaanza kujiuliza ikiwa kweli mwanawe Ukombozi alikufa au amefanyiwa mazingaombwe. Kazi hii ya hadithi fupi imetufaa katika kubainisha sifa kamili za uhalisiajabu ambapo baadhi ya wahusika huwezeshwa hadi kuwashinda wahusika wanaoonekana kuwa wenye nguvu. Ni kupitia kwa hadidhi fupi tumeweza kubaini sifa kama hizo katika wahusika wa tenzi.

## 1.9 Mbinu za utafiti

Utafiti huu umekuwa wa maktaba. Tumesoma mashairi na tenzi mbalimbali za kale. Tumerejelea tasnifu, vitabu, majarida na machapisho mengine ambayo yana makala yaliyotusaidia katika utafiti wetu. Pia tumesoma kuhusu nadharia ya uhalisiajabu na kubainisha sifa zake kutoka maktabani. Tumetumia yaliyomo katika mtandao kuelewa kuhusu nadharia yetu ya uhalisiajabu. Hata hivyo tumepata ushauri mbalimbali kutoka kwa wahadhiri tofauti tofauti, ambao umekuwa wa maana na usaidizi mkubwa kwetu. Kwa sababu moja ya tenzi hizi umeandikwa kwa mtazamo wa kidini, tumewahoji mashehe wa dini ya Kiislamu na tumesoma vitabu vya kiislamu vilivyotusaidia kuelewa tenzi hizi. Hatimaye tulianza uchambuzi wa *Utenzi wa Fumo Liyongo na Ukawafi wa Miiraji.*

### Hitimisho

Mada yetu ya utafiti inahusu uhalisiajabu unavyojitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*, ambapo tumeangazia sifa za wahusika wenye sifa za kushangaza katika tenzi. Kama tulivyotaja hapo awali, machapisho tuliopitia yalikuwa na mchango mkubwa wa uhalisiajabu katika aina nyingine za fasihi huku upungufu ukidhihirika katika tenzi. Utafiti huu utachangia pakubwa katika kudhibitisha kuwa tenzi kama aina nyingine ya fasihi husheheni uhalisiajabu sawia na vipera vingine vya fasihi. Pia utachangia kudhihirisha umuhimu wa uhalisiajabu katika kuendeleza dini, hasa ya kiislamu na ushujaa wa kijamii.

# SURA YA PILI

# HISTORIA YA TENZI NA MATUKIO YA KIAJABU KATIKA *UTENZI WA FUMO LIYONGO* NA *UKAWAFI WA MIIRAJI.*

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia historia ya jamii ambamo tenzi (*Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji* ) zimechipuka. Tumebaini kuwa wahusika katika tenzi hizi wametokana na jamii mbili tofauti. Yaani wahusika katika jamii ambamo *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulitungwa wana sifa tofauti na wale waliomo katika *Ukawafi wa Miiraji*. Tumeonelea ni muhimu kuangazia historia ya jamii ambamo wahusika katika tenzi hizi wamezuka kwani wahusika ndio huunda jamii. Kwa kuangazia jamii zao tumeelewa mazingira walimokulia, vipindi vya nyakati walivyopitia, halikadhalika sifa zao. Kupitia kwa sifa za wahusika hawa ndimo uhalisiajabu hudhihirika. Tumeangazia mazoea ya watunzi wa tenzi kwa ujumla, dhamira katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Mbali na yaliyomo katika *Ukawafi wa Miiraji*, tumeangazia maisha ya Mtume Muhammad tangu kuzaliwa hadi kufa kwake. Tumechukua mtazamo huu kwa sababu mhusika Mohammad ndiye nguzo kuu ya sifa za kiuhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji.*

## 2.1 Historia ya tendi

Wataalamu mbalimbali wametoa fafanuzi zao kuhusu maana na chimbuko la utendi, kwa mfano Abedi (1954:1) anasema kuwa, "ushairi au utenzi ni wimbo, hivyo kama shairi haliimbiki halina maana."Gibbe (1990) akimnukuu Shaaban Robert anasema kuwa ushari ni sanaa ya vina inayopambanuliwa na nyimbo, mashairi na tenzi. Zaidi ya kuwa ni sanaa ya vina, ushairi una ufasaha wa maneno machache au muhtasari. Kwa upande wao Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema ushairi ni "sanaa inayopambanuliwa kwa mpangilio maalumu na fasaha wenye muwala, lugha ya picha, sitiara katika usemi, maandishi au mahadhi ya wimbo ili kuleta wazo au mawazo, kufunza au kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha au mazingira ya binadamu kwa njia inayogusa moyo." Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, ni dhahiri kuwa utenzi umetumiwa kama aina moja ya ushairi. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa, utenzi ni sanaa yenye kuandikwa au kuimbwa kwa kufwata kanuni za ushairi ikiwa na maana kuwa utenzi waweza kuwa wa kimapokeo au wa kisasa

ilimradi ushairi huo uwe na ujumbe. Aidha kutokana na maoni ya wengine tunaweza kusema kuwa, tendi au tenzi ni kisa au hadithi ndefu ya kihistoria inayohusu mtu wa kawaida au shujaa wa kike au kiume aliyewahi kuishi au anayeaminika kuishi. Aghalabu, tendi hugawika katika mishororo minne. Kuna tenzi nyingi katika jamii za Uswahilini. Kati ya tendi hizi ni pamoja na *Ukawafi wa Miiraji, Utendi wa Howani mwana wa Howani, Utendi wa Fumo Liyongo, Utendi wa Mwana Kupona* na nyingine nyingi. Kabla ya kuja kwa wageni, tenzi zilikuwa zinatungwa na kusimuliwa au hata kuimbwa katika sherehe mbalimbali kama vile harusi, jando na tumbuizo anuwai. Mnyampala (1965) anasema kwamba, Waswahili walikuwa wakifungiana nyama kwa kubuni tenzi na mashairi ili kuwasilisha mawazo yao. Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu. Ushairi simulizi wa Waswahili unasemekana kwamba ulikuwepo tangu lugha ya Kiswahili ilipoanza kutumika. Samweli na wenzake (2013), wanamnukuu Mulokozi na Sengo kwa kusema kwamba si rahisi kueleza hasa ni lini ushairi simulizi wa Waswahili ulipoanza. Hali hii ilitokana na sababu kwamba wataalamu mbalimbali wamekuwa na mitazamo tofauti juu ya jambo hilo. Kama Samweli na wenzake (2013), wanamnukuu Knappert (1979) kwa kusema kuwa, ushairi wa mwanzo wa Kiswahili ni Hamziyya ulioandikwa mnamo mwaka wa (1652). Pia wamemnukuu Harries (1995) akidai kuwa ushairi wa mwanzo wa Kiswahili ni Tambuka/Tabuka ulioandikawa mwaka 1728. Hata hivyo utafiti wa Sengo unabainisha kwamba huenda wote wawili (Knappert na Harries) wamekosea kwa kuwa ushairi andishi wa mwanzo wa Kiswahili umekuwapo tangu kuwepo kwa Fumo Liyongo anayeaminika kuishi karne ya 13 huko Pate katika pwani ya Kenya. Aidha utafiti huo unabainisha ushairi wa mwanzo wa Kiswahili ni "Swifa kwa mwana wa Manga" ambao unahusishwa moja kwa moja na Fumo Liyongo.

Gibbe (1980) anasema kuwa tangu kuibuka kwa ushairi wa kwanza hadi sasa, ushairi huo umepitia historia ndefu sana na vipindi tofauti tofauti vya kihistoria. Tunaweza kuvigawa vipindi hivyo katika makundi matatu, kipindi cha kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni. Kipindi cha kabala ya ukoloni kimegawika katika makundi madogo madogo. Kundi dogo la kwanza ni kipindi cha ujima. Kundi la pili ni kipindi cha ustawi wa miji, utamaduni na tawala za Waswahili.

Kipindi cha kwanza cha ujima kilidumu tangu binadamu alipopata urazini na kutoka kwenye uhayawani ikikadiriwa hadi mwaka 600. Inadaiwa kwamba binadamu anatokana na sokwe na alipitia hatua mbalimbali hadi kufikia mtu kamili. Kipindi cha ujima kilianza pale binadamu alipopata urazini na kuanza kuishi kama mtu kamili baada ya kutoka hali hiyo ya usokwe. Katika hatua za awali za ujima, binadamu waliishi kwa uwindaji na ukusanyaji wa matunda. Taratibu binadamu alipiga hatua na kuanza kuyatawala mazingira yake na kuanza kufanya kazi mbalimbali ikiwemo kazi ya kilimo Gibbe (1980).

Mapinduzi haya ya kilimo yalisababisha maendeleo makubwa katika maisha ya binadamu wakaanza kuishi pamoja. Katika kipindi hiki chote cha ujima, mwanadamu alishaibua ushairi kama njia mojawapo ya kujiliwaza wakati wa kufanya kazi. Hakuna ushahidi kuwa katika kipindi hiki kulikuwa na kazi zingine za fasihi. Ushahidi uliopo unaonyesha kwamba hiki kilikuwa ni kipindi kilichotawaliwa na nyimbo za kazi. Hivyo ushairi wa kazi unachukuliwa kuwa ndiyo ushairi wa mwanzo kabisa. Mwanadamu aliimba nyimbo mbalimbali huku akifanya kazi. Senkoro (1988) anasema kuwa, ushairi huu wa awali ambao ulijitokeza zaidi katika nyimbo za kazi uliathiri hisia za mwimbaji kwa kumsukuma kufanya kazi kwa dhati zaidi na kumsahaulisha ugumu wa kazi ile. Nyimbo za kazi ziliendelea kudumu kwa muda mrefu. Hata hivyo sasa kuna mabadiliko makubwa katika utanzu wa ushairi. Nyimbo za kazi (ushairi wa kazi) bado umeendelea kuwa sehemu muhimu ya ushairi wa Kiswahili.

Kipindi cha pili ni kipindi cha ustawi wa miji, utamaduni na utawala wa Waswahili ambacho kilidumu takribani miaka 600 hivi (kuanzia mwaka wa 900-1500 baada ya Kristo). Kipindi hiki kilimalizwa na utawala wa Wareno. Kipindi cha ustawi wa miji, utamaduni na tawala za Waswahili kilidumu kuanzia karne ya kumi na tisa. Kama tulivyoeleza hapo awali, ushairi wa Kiswahili umetokana na ushairi simulizi wa Kibantu. Ushairi huu ulihusisha majigambo, tondozi, pembezi, mbolezi, nyiso, chapuo, nyimbo za kazi na kadhalika. Mulokozi na Sengo kama wanavyonukuliwa na Samweli na wenzake (2013), wanabainisha kwamba kipindi hiki kilitawaliwa na tungo zilizodaiwa kuwa za Fumo Liyongo. Kutokana na wanamapokeo tunaambiwa ya kwamba mshairi wa kale zaidi anayefahamika ni Fumo Liyongo, ambaye aliishi takribani karne ya 13. Ingawa inaaminika kuwa Liyongo aliishi kabla ya Karne ya 16,

kuna tungo zinazomhusu (ziliandikwa na wengine) ziliandikwa mwanzoni mwa karne ya 19. Tungo hizo ni takhmisa ya Liyongo (Sayyid Abdalla bin Ali inayokadiriwa kuandikwa 1800) na "Utenzi wa Fumo Liyongo" (Muhamadi kijumwa 1913). Katika utafiti wetu tunaunga mkono maoni ya Sengo kwamba Fumo Liyongo ndiye aliyewahi kutunga ushairi wa mwanzo kabisa. Aidha tunakubaliana na wazo kuwa ushairi wa mwanzo ulianza kama nyimbo za kazi. Tungo hizi za awali, zilitokana na fasihi simulizi inayomhusu Liyongo na iliyotungwa na Liyongo mwenyewe.

Kwa hivyo *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni miongoni mwa tenzi tatu za kale. Tenzi zingine mbili ni Utenzi wa *Mwana Kupona* na *Utenzi wa Ali Inkishafi.* Madai haya yameungwa mkono na Mulokozi (1999) *Tenzi tatu za kale*. Utenzi wa Fumo Liyongo kwa mfano unaeleza kuhusu kustawi kwa mji wa Pate alipoishi Liyongo. Utenzi huu ulitungwa kutokana na hadithi za kimapokeo kuhusu Liyongo mingoni mwa Waswahili. Hata hivyo masimulizi ya maisha ya Liyongo kama yanavyotokea katika utendi huu si kamili bali ni simulizi mojawapo ya maisha yake. Masimulizi mengine yametokea katika nyimbo zake. Kwa kutafitia *Utenzi wa Fumo Liyongo*, ni wazi kuwa utafiti wetu umeangazia mojawapo ya tenzi za kale zaidi zilizowahi kuchapishwa.

## 2.2 Historia ya Waswahili.

Historia ya Waswahili ina msingi wake katika visasili na visakale. Mwazoni Waswahili hawakujua kuandika wala kusoma. Kwa hivyo fasihi yao ilihifadhiwa akilini mwa wenyeji. Hivyo ilipitishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya midomo. Maelezo ya maisha ya Waswahili yalianza kutiwa katika maandishi kwa mjo wa Waarabu. Wazungu walichangia pakubwa pia katika kuhifadhi historia ya waswahili katika maandishi kama vile Werner (1915), Dammann (1940), Greenville (1954), Lyndon (1962), Sutton (1966), Knappert (1970), Allen (1977), Nurse na Spear (1985), Nurse (1994), miongoni mwa wengine. Wageni hawa walikusanya mila, desturi na tamaduni za Waswahili kutoka kwa wenyeji wa pwani na kuzihifadhi katika maandishi.

Waswahili wana asili yao kama yalivyo makabila mengine. Asili yao ni katika eneo ambalo hivi sasa linakaliwa na nchi ya Cameroon na eneo la Mashariki mwa nchi ya Nijeri. Nurse na Spear (1985) wanatoa rai kuwa baadhi yao walihamia katika janibu za Kusini mwa Afrika, ilihali wengine wakiwemo Waswahili, walihamia Mashariki

na kukalia eneo la Shungwaya. Kuna madai kwamba chimbuko lao ni Shungwaya upande wa Somalia. Kwa upande wao wanamapisi mapokezi wana maoni tofauti kwamba Shungwaya kamwe hapakuwa chimbuko la Waswahili. Kulingana nao wanasema kwamba kuna Shungwaya tatu: Shungwaya ya juu, ya chini na Shungwaya ya kati. Shungwaya ya juu ilikuwa ya Wagalla, ya kati ilikuwa ya Wamijikenda na Shungwaya ya chini ikawa ya Waswahili. Makundi haya matatu ndiyo yaliyokuwa yakiishi Shungwaya. Tunaunga mkono maoni ya wanamapisi kuwa kuna Shungwaya tatu ambazo ndizo chimbuko hasa la Waswahili. Kundi la Wagalla ndilo lililokuwa na nguvu za kivita na hivyo kuwatesa wenzao. Kutokana na vita baadhi yao walisalia ilihali wengine wa kabila la Watikuu lilianza kutafuta maskani mapya katika Visiwa vya Birikavo, Chula, Chovae na Mdowa. Wenzao pia walifululiza mpaka wakafika Kiunga, Wakasambaa wakavuka Kiwayuu, Ndau na kisiwa cha Pate, wakakaa Kizingitini, Mbwajumwali, Chundwa na Nyabogi na wengine Faza.

Nurse na Spear (1985), wanaendelea kusema kuwa, kundi la Wa-Mijikenda lilipitia njia ya msituni mpaka wakafika mto Tana ambapo kulikuwa na mji wa Wagalla. Mji huu ulikuwa umezungukwa na boma na katika lango kuna walinzi. Wamijikenda waliufikia mji huu usiku ambapo waliwaua walinzi na wakaingia katika mji. Walipoingia waliwaua Wagalla wengi sana na wengine wakatoroka, hivyo mji ukashikwa na Wamijikenda. Kundi lililosalia lilijiita Wapokomo, wengine waliendelea hadi wakafika Malindi upande wa juu kupitia Marafa, Chakama, Ganda na Jilore. Kundi hili la watu lilijiita Wagiriama.

Kabila la mwisho liliendelea na safari likafika Mombasa na kuvuka upande wa Likoni. Kikundi hiki kilikuwa kimechukua chombo ambacho walikiabudu. Walipofika Likoni chombo hicho kikaanguka na kuvunjika kwa mlio au mshindo. Ni kutokana na mlio huo ndipo jina lao likachipuka na hivyo wakajiita Wa-digo. Baada ya hapo baadhi yao waliendelea na safari yao wakaingia upande wa Tanganyika. Hadi hii leo Wadigo wamo Kenya na Tanzania.

Frawley (2003), anaelekea kukubaliana na maoni yao Nurse na Spear (1985) , kuhusu chimbuko la jamii ya Waswahili. Kwa ujumla jamii ya Waswahili imepitia vipindi mbali mbali vya kihistoria huku maisha yao yakijawa na mapambano ya vita vya mara kwa mara. Vita hivi vilikuwa baina ya makabila yao na wakati mwingine

walivamiwa na majirani pamoja na wageni kama vile Waarabu. Watu wengi waliaga dunia na mali yasiyokadirika kupotea. Hili lilipelekea wao kupata hasara kubwa mno. Wenyeji wa bara kama vile Walanguo, Wadahalo, Wasegeju, Wasanye na Wagalla waliwashambulia sana Waswahili. Waswahili walijawa na huzuni, taabu, hasara na hata maafa. Kutokana na changamoto hizi ndipo walikuwa na hamu kuu ya kutaka kupata mtu ambaye angewasaidia kuleta umoja, maelewano undugu na ushindi katika vita. Katika kipindi cha changamoto nyingi, Fumo Liyongo anazaliwa. Ni maoni yetu kuwa huenda Waswahili walimhitaji Liyongo kwa dhati ili awatatulie changamoto hizo. Liyongo anapozuka kila kabila linadai eti ni wao kwa sababu kila mojawapo ya kabila hizo walikuwa na changamoto na walihitaji mtu wa kuwatatulia.

### 2.3 Mazoea ya waandishi wa tenzi.

Katika *Ukawafi wa Miiraji*, ubeti wa kwanza hadi wa pili, mtunzi anatoa dibaji fupi kwa kutaja sifa za Muumba. Anamtolea muumba sifa zisizo kikomo kwa ukuu wake. Kisha anakamilisha ubeti wa pili kwa kutuma salamu kwa Mtume Muhammad na ukoo wake. Hatimaye anaanza kusimulia hadithi ya kisa cha *Miiraji* kuanzia ubeti wa tatu. Mtindo sawia umedhihirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, ambapo mtunzi anatanguliza kwa jina la Mwenyezi Mungu na kwa jina la Muhammad kama njia ya kushukuru na kuomba baraka ili awezeshwe kuwaandikia wazaliwa watakaokuja baada yake. Hatimaye anaomba karatasi, wino mweusi na meza ambavyo ni vifaa faafu vya kuandikia. Katika ubeti wa nne, mtunzi anabainisha dhamira yake ya kutaka kuyaandika yaliyomfika Liyongo. Ni maoni yetu kuwa fomula hii, inadhihirisha chimbuko lake na athari za hati ya Kiarabu katika tendi. Hili halina budi kutokea kwa sababu, Waarabu ndio waliowafundisha Waswahili kusoma na kuandika kwa kutumia hati za Kiarabu.

### 2.4 Kisa katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*

*Utenzi wa Fumo Liyongo* unahusu mgogoro kati ya Fumo Liyongo na kaka yake, sultan wa Pate ambaye hajatajwa kwa jina. Mwanzoni utenzi unamdokeza Liyongo akiwa ana umri wa makamo hivi, aidha kimo na nguvu zake za mwili ziliwashangaza wengi kwa hivyo walimsifia mno. Watu wa kabila la Wagalla walipofika Pate kutafuta chakula ili wanunue, walielezwa sifa za Liyongo na wananchi, halikadhalika Sultani wa Pate alimsifu Liyongo. Kwa kusikia sifa hizo za ajabu Wagalla walitamani

sana kumwona Liyongo, kwa hivyo Sultani akamwandikia Liyongo waraka akimwomba aje ili Wagalla wamwone.

Liyongo akaitikia wito huo, hivyo akapanga safari yake ya kwenda Pate huku amebeba mizigo chungu nzima. Kati ya vitu alivyovibeba ni panda, kinu na mafiga. Kwa mwanadamu wa kawaida, safari hiyo ni ya siku nne lakini Liyongo alichukua siku mbili tu na kufika Pate. Alipokaribia jijini Pate, alipuliza panda ya kwanza hadi ikapasuka. Alipuliza ya pili nayo vile vile ikapasuka. Alipuliza ya tatu na kuingia mjini hadi barazani kwa sultani. Watu walishangaa mno kwa sauti kubwa ya panda. Watu wengi wakakusanyika kumwona, alipotua mzigo wake, ulikuwa umejaa vitu vingi ambavyo vilitosha kuijaza nyumba nzima. Moja kwa moja, Wagalla wakakiri kuwa kweli Liyongo ni mtu mnene na mwenye nguvu.

Wagalla wakatamani sana kuipata mbegu yake, hivyo walimwomba sultani awaruhusu kupata mbegu hiyo; Sultan alimuuliza Liyongo naye akaridhia. Wakafanya mpango wa kumwoza mke wa Kigalla ambaye alimzalia mtoto wa kiume. Sifa za Liyongo zilivyozidi kusambaa ndivyo mgogoro kati yake na Sultan wa Pate ulivyozidi. Mfalme alihofia kuwa huenda Liyongo angemnyang'anya ufalme hivyo akatafuta njia ya kumwangamiza. Liyongo alipogundua njama ya Sultan ya kutaka kumwangamiza, akatoroka Pate na kwenda kuishi nyikani pamoja na Wadahalo, Watwa, Wasanye na Waboni. Mfalme akafanya mpango wa kisiri pamoja na Wasanye na Wadahalo ili wamuue huko mwituni kwa kuwaahidi malipo ya reale mia moja iwapo wangemletea kichwa cha Liyongo. Watu hao walifanya urafiki na Liyongo kisha wakashauri wawe wakicheza kikoa pamoja. Hivyo walichaguana kwa kupeana zamu ya kuangua makoma kutoka mtini. Walipanga kuwa ikifika zamu ya Liyongo, wamngojee apande mkomani kisha wamfume kwa mishale yao wamuue akiwa mtini. Kwa uwezo wa kiakili aliokuwa nao Liyongo, akagundua njama hiyo. Badala ya kupanda mtini aliangua makoma akiwa chini aridhini hivyo wakashindwa kumuua.

Watu hao walimpelekea Sultani ripoti kuwa haiwezekani kumuua Liyongo. Mfalme aliwaambia warejee alipo Liyongo wamweleze kuwa mjini ni salama na hapana hatari yoyoyte ili waende naye huko. Waliporudi wakamweleza Liyongo uwongo huo ambao aliuamini kuwa kweli, kwa hivyo akawafuata na kuenda nao mjini Pate. Sultan

akaandaa ngoma ya gungu na mwao na kuwaalika wapenzi wa aina hizo za ngoma, Liyongo alikuwa mmoja wao. Ngoma iliposhika kasi, askari walimnasa Liyongo na kumtia korokoroni. Mfalme na watu wake waliamua kumuua Liyongo akiwa gerezani. Siku ya mauaji kutekelezwa ilipokaribia, Liyongo akapewa muda wa kutoa ombi kwa kitu chochote apendacho. Liyongo akaomba apigiwe ngoma ya mwao na gungu. Ombi hili likakubaliwa na ngoma ikaandaliwa. Ngoma ilipoandaliwa, Liyongo akatuma ujumbe wa kishairi kwa mama yake kupitia kwa kijakazi Saada ambaye humletea chakula. Katika ujumbe huo alieleza kwamba siku hiyo ya ngoma apike mkate wa wishwa na ndani yake atie tupa ya kukatia minyororo. Mama yake akafanya vivyo hivyo. Kijakazi Saada alipompelekea chakula, walinzi wakachukua mikate waliyodhania kuwa mizuri na kuutupilia mbali ule wa wishwa ili umwendee Liyongo. Ngoma iliposhika kasi, Liyongo akatumia nafasi hiyo kukereza minyororo, hivyo akafaulu kuikata. Akavunja Lango kuu la jela na kutorokea msituni.

Mfalme alipoona kuwa ameshindwa kumuua Liyongo, akamshawishi mwanawe Liyongo aende amuulize babake kiwezacho kumdhuru. Sultani alimpa ahadi ya kumwoza bintiye, kumpa uwaziri katika uongozi wake na mali nyingine ikiwa angefanikiwa. Mwanawe Liyongo akafululiza hadi Shaka alipokuwa babake na kumtaka amweleze siri ya yeye kutodhurika na kitu chochote. Ingawa Liyongo alitambua njama ya mahasidi wake ya kupitia kwa mwanawe, alikubali kumfichulia siri. Alimweleza kuwa kiwezacho kumuua ni sindano ya shaba ikitiwa kitovuni mwake. Sultan alijawa na furaha sana, alipopewa taarifa hii na kijana huyu wa Liyongo. Kwa hivyo akampatia sindano ya shaba, akampa ahadi zaidi na kumpa zawadi tele. Akarejea Shaka tena alipo babake, akamngoja alipokuwa usingizini, akamchoma sindano ya shaba kitovuni. Liyongo alizinduka na kuamka kwa hasira, akachukua mshale wake na kuelekea kisimani akimtafuta adui . Akiwa amepiga goti, akatia mshale katika upinde huku akiuelekeza mjini na kukata roho. Umati wa watu walipomwona akiwa katika hali hiyo, wakadhani yuko hai na kaudhika mno. Kwa hivyo walijawa na hofu ya kwenda kuchota maji kisimani. Walipozidiwa na ukosefu wa maji, walikwenda kumwomba mama yake Liyongo aje ambembeleze aondoke wateke maji. Mama yake akawa anaenda kumbembeleza mara kwa mara lakini alikosa kufanikiwa. Hatimaye maiti yake iliaanguka ndipo watu wakabaini kuwa alikuwa ameshakufa.

Sultani alipopata habari ya kifo cha Liyongo alijawa na furaha. Akamwarifu mwanawe Liyongo kuwa babake amefariki. Badala ya kuwa na masikitiko, huzuni na maombolezo, yeye alifurahi. Kitendo hiki kinamuudhi mfalme ambaye alichukua mali yote aliyokuwa amempa. Wanajamii wakamfukuza kijana huyu asitangamane nao. Siku chache baadaye akakumbana na maradhi yasiyokuwa na tiba ambayo yalimwangamiza.

### 2.5 Usuli wa Mtume kabla ya Miiraji

Mtume Muhammad alizaliwa katika familia ya kibepari. Ukoo wake ulinawiri na kuwa na ushawishi mkubwa. Babake anaaga dunia muda mfupi tu kabla ya kuzaliwa kwa Mtume. Mamake pia anaaga dunia na kumwacha mwanawe akiwa na umri wa miaka sita. Anabaki mikononi mwa babuye ambaye anaitwa Abdul Muttalib. Kabla ya kifo chake anamkabidhi mjukuu wake kwa ami yake aitwaye Abu Talib. Mtume akawa anachunga mbuzi katika mji wa Makkah na alipotimiza miaka kumi na miwili akawa anasafiri na ami yake kwenda Sham kwa ajili ya biashara. Sifa njema za Mtume zilinawiri sana akawa alijulikana hasa kwa uaminifu wake. Kutokana na tabia njema aliyo nayo, mjane Khadijah alimwamini Muhammad, hivyo anamwacha katika nafasi ya kuendesha biashara yake. Alipohitimu umri wa miaka ishirini na mitano, alimwoa Khadijah. Kwa miaka takriban kumi na mitano hivi alifanya biashara na kufaulu vyema, hivyo aliishi maisha ya mfanyi biashara. Kadri muda ulivyopita, tabia yake ilibadilika na kuanza kuwa na tabia fulani isiyo ya mfanyi biashara.

Muda baada ya muda angejiendea milimani kwa taamuli ya kibinafsi na maombi ya kipekee. Takribani katika miaka ya 610 alikuwa na maono ambayo yalibadilisha maisha yake na historia ya dunia. Alipokuwa katika mlima Hira malaika mkuu alimjia. Malaika huyo alipoondoka Mtume anaeleza baadaye alivyosakamwa kooni huku akiamrishwa kulitamka jina la Allah. Tukio la Mtume kukutana na malaika mkuu lilitokea mara kadhaa baadaye maishani mwake. Mnamo miaka ya 613, Muhammad alihubiri kule Makkah kuhusu ujumbe aliokuwa amepokea. Ujumbe huo ulihusu uwepo wa Mungu ambaye ni mwenye uwezo mkuu na mwenye huruma. Pia aliwatambua mitume wengine hasa Ibrahimu, Musa na Isa ambao mbeleni walikuwa wameshahubiri ujumbe kama huo wake.

Kuabudu kwa Mungu mmoja si jambo lililofahamika sana miongoni mwa waabudu miungu, lakini muda ulivyoendelea kupita ndivyo Mtume alivyopata wafuasi wake na wakati huo huo akawa na maadui miongoni mwa wafanyi biashara wa Makkah. Mnamo 622 maadui wake walipanga njama ya kumuua. Kutokana na hili alitoroka kuelekea mji wa Yathrib ambao ni mji ulio takriban kilomita mia tatu kaskazini mwa Makkah.

Watu wa Yathribu-kundi dogo lililofanikiwa, walimkaribisha Mtume na wafuasi wake. Mnamo 622 dini ya Kiislamu ilianza kuimarika jijini Yathribu. Enzi za uislamu zilijulikana kuwa nyakati Mtume aliondoka Makkah, ambapo kulingana na kalenda ya waislamu huo ukawa ndio mwanzo wa mwaka wa kwanza. Mji wa Yathribu ulibadilishwa jina na kuitwa Madinat al-Nabi, lenye maana ya mji wa Mtume na hivyo mji huu ukaja kujulikana kama Medina. Alipokuwa huko Mtume alipata wafuasi wengi kila uchao. Watu hao walikuwa ni wa kidini, viongozi wa kijeshi mbali na mabepari watajika. Mtume anabaki bila mke kwani Khadija anafariki katika mwaka wa 619.

Mtume aliendelea kuhubiri na kutamka maneno anayofunuliwa na Mungu. Wafuasi wake walikusanya matini pamoja na maono ya Mtume aliyopokea akiwa kule Makkah. Maono hayo ya Mtume na maneno aliyoyahubiri baadaye yaliandikwa na kuwa Kuran Tukufu. Matini ya Kuran iliyoidhinishwa kuwa kamili ni ile iliyoandikwa na mfuasi Othman wa tatu mnamo 650. Mahusiano ya Mtume na watu wa Makkah yaliharibika hadi vita vikazuka kati yao. Mtume aliwaongoza watu wake katika vita. Walipigana vita vikali hadi kundi la mtume Muhammad linaibuka mshindi. Mnamo 629 Mtume aliwarai tena watu wa Makkah kumruhusu yeye na jeshi lake warejee ndani ya mji huo ili kutekeleza ibada ya haji. Katika kutekeleza ibada ya haji, wafuasi wa Mtume waliwafurahisha wenyeji kwa kuondoka baada ya siku tatu za haji kama walivyokubaliana. Mwaka uliofuata watu wa Makkah waliwachokoza waislamu, kitendo hicho kiliwakasirisha kiasi cha wao kundamana ndani ya Makkah. Waislamu hao waliudhibiti mji wa Makkah kwa urahisi mno. Hatimaye Wenyeji wa Makkah walislimu. Mtume alitumia fursa hiyo kuiondoa miungu yote na kuacha kaaba pekee. Muhammad alitoa msimamo kuwa Kaaba ndio itasalia kuwa kigezo muhimu katika dini ya Kiislamu. Hivyo Makkah ilikuwa jiji kuu takatifu la dini ya kiislamu. Baada ya mapatano ya amani na wenyeji wa Makkah,

Mtume aliishi miaka miwili pekee kisha akaaga dunia. Mtume hakuwa na mwana wa kiume aliyeishi hadi ukubwani. Wanawe wa pekee waliosalia ni wa kike ambao Khadijah alimzalia. Aliwahi kuwaoa wake wengine kabla ya kifo chake. Kati ya wake wake wote, Mtume alimpenda sana Aisha.

## 2.6 Kisa cha Miiraji.

Katika usiku mpevu, Mtume alikuwa amelala alipokuwa anaianza kazi yake ya utume. Utenzi unadokeza kuwa paa la nyumba ya Mtume lilipasuliwa wazi na malaika watatu wakamjia; Mikaili, Jiburili na malaika mwingine ambaye hajatajwa. Walimwamsha Mtume na kumbeba hadi kwenye kisima cha Zamzam ambapo walimlaza. Malaika Jibrili alimfungua kifua cha Mtume ili akitakase. Baada ya kumaliza akakishona vyema bila alama ya kushonwa kuonekana, hatimaye akamtia Mtume mhuri wa utume. Muhammad alipoamka, akaona mnyama kama farasi mweupe mwenye umbo la ajabu kabisa na sifa za ajabu ambazo hajawahi kuona maishani mwake. Farasi huyo alikuwa tofauti na farasi wengine. Farasi alikuwa na uso wa kibinadamu, lakini mashavu yake yalikuwa ya ki-farasi; macho yake yalikuwa kama jiwe lenye thamani sana huku yanang'aa kama nyota. Mwili wake ulikuwa umejaa johari na majiwe mazuri yenye thamani. Kutokana na ule mwendo wa kasi kabisa aliitwa buraki. Mnyama alijongea na kujituliza ili Mtume amkalie. Alipaa hadi juu kabisa; juu ya milima ya Makkah. Wakiwa milimani, Malaika mkuu aliwaamrisha kurejea aridhini ili Mtume aongoze sala, hivyo walirudi juu ya aridhi na Mtume akaongoza sala. Wakaendelea na safari hiyo wakafika katika lango la msikiti wa Jerusalemu. Kutokana na nuru ya buraki, Mtume aliweza kuona vizuri akaingia hadi msikitini, aliwaona mitume Ibrahimu, Musa, Issa na wengineo. Baada ya yeye kuwaswalisha, mara nuru iliteremka kutoka mbinguni ikiwa katika hali ya ngazi ambayo ncha yake ya mwisho iligusa na kuegemea juu ya Shakra au jiwe la msingi la nyumba tukufu. Akisaidiwa na malaika Jibrili, Mtume anapanda ile ngazi na kuendelea na safari yake.

Mtume aliwasili katika mbingu ya kwanza, baada ya kufika mbingu hii, malaika Jibrili akabisha lango. Lilipofunguliwa wakaingia ndani, Mtume akajongea ndani, akakaribishwa na mtu wa kale. Malaika jibril alimweleza Mtume kuwa mtu huyo ni Adam, akaambiwa amtolee heshima na bila kusita Mtume akafanya hivyo. Adamu alimkumbatia Mtume huku akimwambia kuwa yeye ni mkuu wa wana wake wote na

wa kwanza kwa mitume wote. Katika mbingu hii ya kwanza kuna wanyama wa kila aina. Wanyama hao walikuwa malaika walioomba wafanane na wale waliomo aridhini. Miongoni mwa wanyama hao ni ndege mwenye urefu wa kushangaza, kishungi chake kilikuwa kinagusa mbingu ya pili, ingawaje ni safari ya miaka mia tano kutokea ile mbingu ya kwanza. Huyo ndege wa ajabu alikuwa anaimba kila siku kwa sauti yake tamu kila asubuhi. Wanyama wote waliomo aridhini wanaomsaidia binadamu huamshwa na sauti yake, aidha wale ndege wa kundi lake hufuatisha sauti yake.

Mtume aliwasili katika mbingu ya pili, kama mbingu ya kwanza, Jibrili alibisha mlango uliofunguliwa. Humo walikutana na Mtume Nuh ambaye alimpokea, akamkumbatia na kumweleza kuwa yeye ni mkuu kuliko mitume wote waliotangulia. Walielekea mbingu ya tatu, walipokewa vyema, hapa walipata malaika ambaye hapimiki kwa ukubwa. Nafasi kati ya Jicho moja na lingine ilikuwa umbali wa kiasi cha safari ya siku elfu sabini. Yeye alikuwa na vikosi vya mamia ya maelfu ya watu ambao walikuwa wanasubiri amri yake. Mbele yake kulikuwa na kijitabu kikubwa kweli kweli ambacho kila mara alijishughulisha katika kukiandika, kupekua pekua na kufutilia mbali mengineyo. Jibrili alimweleza Mtume kuwa huyo alikuwa Izrail; malaika wa vifo ambaye yuko katika amri ya Allah. Alimweleza zaidi kuwa katika kitabu hicho, alikuwa anaandika majina ya wale watu waliokwisha hitimisha maisha yao au kufikia wakati wao na ambao walishafariki.

Walifika mbingu ya nne, miongoni mwa malaika waliokuwa huko kulikuwa na malaika ambaye alikuwa mkubwa; kuanzia kichwani hadi miguuni ilikuwa umbali wa safari ya miaka mia tano. Uso wake ulipokunjika ulitiririsha mito ya machozi yaliyobubujika mno. Malaika huyu aliwateua wana wa Adamu wanaotenda dhambi na kuwabashiria maovu yaliyowasubiri.

Walienda mbingu ya tano, Mtume alipokelewa na Mtume Haruni huku akipongezwa na malaika waliotawala moto. Kati ya malaika hao Mtume alikutana nao, Mustafa ni malaika mmoja wao alitisha sana kuliko wenzake wote. Uso wake ulikuwa wa shaba, alikuwa amevikwa/funikwa kwa visugu. Macho yake yalikuwa yanang'aa kama radi na alikuwa ameushika moto. Yeye alikuwa amekalia kiti kilichozungukwa na moto, mbele yake kulikuwa na minyororo miekundu kwa sababu ya moto. Ikiwa angefika

aridhini basi milima yote ingeyeyuka, maziwa na bahari kukauka na viumbe vyote kufa kwa vishindo vyake. Malaika huyu na mawaziri wake ndio walipewa amri ya kuteremsha adhabu ya moto kwa makafiri na watenda dhambi.

Wakiacha ya kutisha, waliwasili mbingu ya sita, hapo walimwona malaika mkubwa kabisa upande mmoja alikuwa theluji na nusu iliyosalia alikuwa moto. Hata hivyo theluji haikuyeyuka wala moto kuzimika. Malaika Jibrili alimweleza Mtume kuwa huyo alikuwa mlezi wa malaika wa mbinguni na aridhini. Hapo palikuwemo na Mtume Musa, badala ya kumkaribisha Mtume kama wengine, yeye alilia sana kwa sababu Malaika Jibrili aliandamana na Mtume ambaye angewaelekeza watu kuingia peponi.

Walielekea mbingu ya saba, ambapo alilakiwa kwa furaha nyingi na mtume Ibrahimu, mzee mkuu mwenye heshima. Katika mbingu hiyo palikuwa pamejaa mwanga wa nuru na kudura ya Allah. Sifa ya mbingu hiyo hakuna mdomo unaoweza kueleza. Malaika huyu mmoja anatosha kumwaya mwanga juu ya malaika wengine. Yeye aliigawa dunia katika mistari mirefu sambamba, na alikuwa na vichwa elfu sabini na kila mdomo ulikuwa na ndimi elfu sabini, na kila ulimi ulisema lugha elfu sabini mbalimbali: haya yote yalisemwa katika kumsifu Allah. Mtume akiwa katika hali ya mshangao kwa haya, mara alivutiwa na mmea ulioitwa Sarat ambao ulinawiri vyema kwa upande wa kulia mwa kiti cha enzi cha Allah. Matawi yake yalisambaa zaidi ya umbali wa kati ya jua na ardhi. Malaika walikuwa wengi zaidi ya mchanga wa pwani. Malaika hao walifurahi chini ya kivuli cha mti huo, wote wakiwa wanasoma aya za Kurani tukufu. Majani ya mti huo ni sawa na masikio ya tembo, matunda yake yalikuwa makubwa kama mitungi, matunda ya mti huo yalikuwa matamu na meupe kuliko maziwa. Mti huo ulipogubikwa na amri za Allah, ulibadilika na kuwa katika hali ambayo hakuna kiumbe anaweza kuufananisha kwa uzuri wake. Kulikuwa na mito minne karibu na mti huo: Miwili ikiwa haionekani na miwili ikiwa wazi yaonekana. Mtume alielezwa kuwa mito miwili isiyoonekana ni ya peponi na inayoonekana ni mto Naili na Furati.

Mtume Muhammad waliongozana na Jibrili hadi nyumba ya kusujudia, iliyokuwa na sifa za kupendeza sana. Nyumba ilijengwa na mawe sita ya njano, pia ilizungukwa na taa chungu nzima zilizokuwa zikiwaka. Mtume alikaribishwa ndani, mlimokuwa

vyungu vitatu; kimoja kilikuwa kimebeba pombe, kingine maziwa na cha mwisho asali. Mtume anachagua maziwa na kuyanywa. Malaika Jibrili alimpongeza kwa kuyanywa maziwa. Alimweleza pia ikiwa angekunywa pombe umma wake ungeangamia. Nyumba hiyo tukufu ililingana na kaaba ambayo iko Makkah. Wakati huo malaika walikuwa wakilizunguka jumba hilo mara saba, mtume Muhammad akajiunga nao.

Walifika mahali ambapo Malaika Jibril hawezi kusonga mbele kwani hapo ndipo palikuwa kikomo chake. Muhammad aliendelea peke yake, akiwa mwepesi hata kuliko mawazo, alipitia katika uwanja mkubwa uliogawika mara mbili; eneo moja la uwanja huo liliwaka taa na lingine lilijaa giza tupu. Alizidiwa na woga na ukimya kwa sababu ya kuwa pweke. Mara hii alijiwa na wimbi la furaha, yaliyofuatia ni manukato mazuri yaliyonuswa na Mtume pekee. Mtume alipewa sala hamsini kwa ajili ya umma wake. Alirejea na agizo hilo, alipofika mbingu ya sita, alikutana na mtume Musa ambaye alimshauri arudi kwa Mola wake amuombe ili apunguze sala hizo. Mtume alirudi kwa Mola wake na akampunguziwa sala kumi, aliposhuka katika mbingu ya sita, alikutana na mtume Musa tena. Mara hii mtume Musa alimrudisha kwa mola wake ili sala hizo zipunguzwe zaidi. Mola alimpunguza sala kumi, aliposhuka kwa mtume Musa, alimwambia arejee kwa Mola wake, Mtume alifanya hivyo tena na tena hadi sala hizo zikapunguzwa zikabaki tano kwa siku. Alipoambiwa arejee kwa Mola zipunguzwe zaidi, Mtume alisema kuwa ameaibika mno kurudi tena kwa Mola wake. Akiwa na sala tano,alishikilia ile ile ngazi ya nuru ambayo ilikuwa imemleta hadi mbinguni, Mtume alishuka hadi msikiti wa Baitil Madqis hapo Jerusalemu na kukutanishwa na Nabii Ibrahim na Nabii Musa na Nabii Isa pamoja na manabii wengine wakiwa wamekusanywa kwa ajili yake. Mtume akasimama kuwasalisha kisha akatoka na kupanda buraki na kurudi Makkah usiku ule ule. Asema mwenyezi mungu:

> Akamfunulia mja wake aliyomfunulia.
> Moyo haukusema uwongo uliyoyaona.
> Je! Mnabishana naye kwa aliyoyaona?
> Na akamwona (Jibril kwa )mara nyingine,
> penye mkunazi wa mwisho.
> Karibu na hapo ipo Bustani inayokaliwa,
> Kilichofunika huo mkunazi hicho kilichofunika,
> Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka,
> Kwa yakini aliona katika ishara kubwa kabisa za mola wake
> (Sura: An-Najm:10-18)

Katika utafiti wetu, mawazo yetu yalivutiwa na idadi ya sala kwani ndicho kiini hasa kilichompeleka Mtume katika mbingu ya saba. Aidha Mtume anarejea kwa Allah mara kadhaa ili sala hizo zipunguzwe. Ni wazi kuwa utenzi huu umeegemea katika dini ya Kiislamu ambapo sala ni kiungo muhimu. Kwa kuzingatia kigezo cha sala, ni maoni yetu kuwa Mola haweki sheria yoyote isipokuwa iwe na maslahi ndani yake. Kwa mantiki hii Mtume hangehitaji kurudi kwa Mola wake mara hizo zote kwa ajili ya kupunguziwa sala. Kwa sababu Allah ana upendo kwa umma wa Mtume, tunakisia kuwa hata kama Mtume angemsihi mola mara moja tu apunguze sala hizo hadi tano, basi Mola angetekeleza. Sababu ya kufanya hivyo ni kutaka kuwepo na sheria zilizo na masilahi, kwani mtume Musa anaamini kuwa sheria hii ya sala hamsini kwa siku ingekuwa ngumu kutekeleza.

## 2.7 Dhamira katika *Ukawafi wa Miiraji.*

Wamitila (2003) anasema, dhamira ni istilahi inayotumiwa kuelezea wazo kuu katika hadithi, riwaya, tamthilia, hadithi fupi, shairi n.k. Wazo hilo kuu huhusiana na lengo la mwandishi wa kazi hiyo. Huweza pia kutumiwa kuendeleza lengo kuu la utunzi. Ni suala linalokuzwa na kuendelezwa na msuko pamoja na mahusiano ya wahusika mbalimbali katika kazi ya kifasihi. Tunaunga mkono madai ya mtalaamu huyu, kwa hivyo tumechukua mtazamo wake tulipoangazia dhamira katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

Mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* anaeleza safari ya mtume Muhammad aliyeongozwa na Malaika Jiburili kwenda Jerusalemu na kupanda katika mbingu saba kupitia Miiraji (ngazi). Ni maoni yetu kuwa lengo la safari hii lilikuwa kumtayarisha Mtume kwenda kukutana na Muumba wake ili apokezwe sala. Kabla ya safari kuanza, Mtume alipasuliwa kifua, akatolewa nyongo, akaoshwa na uovu wote ukatolewa, akaandaliwa tayari kwa safari.

Dhamira ya mtunzi wa *Ukawafi wa Miiraji* ilibainika pale ambapo, Mola alimweleza Mtume kuwa yeye ndiye bora zaidi ya Musa, Isa, Haruni na mitume wengine. Anamweleza kuwa umati wake Muhammad ndio afadhali kuliko wote. Mtunzi alidhamiria kuwaelezea wasomaji na wafuasi wa dini ya Kiislamu kuwa, mtume Muhammad ndiye aliyeteuliwa na Mwenyezi Mungu:

Na kamaye Isa akipoza kula kilema,
Na kuwafufua wafieo yake kalmia,
Nawe nikupele kufufua na mangi kama,
Ni yako kanizi ya arisi isiyokoma (ubeti wa 81).

Mtume Muhammad pekee ndiye aliyeweza kuonana uso kwa uso na Allah wake. Hata malaika Jubiril hakufika kipeo alichofika Muhammad. Aliachwa nyuma Mtume akafunikwa na kiwingu cha rehema yake Jalali. Muhammad ndiye aliyeleta neno moja kwa moja kutoka kwa Mungu hadi kwa binadamu. Mitume wengine hawakupewa uwezo kama alivyopewa mtume Muhammad. Kwa mfano, Isa aliweza tu kupoza na kufufua wafu. Mtume Muhammad akapewa uwezo huo na zaidi. Jina la Mola linapotajwa, la Muhammad linatajwa pia. Ili kudhihirisha kuwa mtume Muhammad ni mteule, mtunzi anatueleza kuwa, Makureishi walipomwuliza kuhusu watu wao waliokuwa safarini, Mtume aliwaahidi kuwa wangefika Ijumaa ya tano. Ilifika Ijumaa hiyo ambayo Mtume alikuwa amesema bila watu hao kuonekana. Mtume alimuomba Mola ashikilie jua hadi watu wale wafike na Mola akamtimizia:

Wote Makureshi wakanena:Ai amini,
Ndizo swifa zake umeziye kuzibaini,
Tuna watu wetu safarini, bani fulani,
Watakuya lini,utwambie tukifahama (ubeti wa 105).

Muhammad ndiye aliyeongoza mitume wote katika sala, ndiye Imamu mkuu. Katika *Ukawafi wa Miiraji* tunaelezwa tukio lililo muhimu zaidi katika maisha ya Mtume. Mwandishi anaeleza asili ya uisilamu. Hii ni nguzo muhimu ya dini ya Kiislamu. Inaelimisha wasomaji/wafuasi wake kuhusu kuwepo kwa pepo na jahanamu.

Mtume alionyeshwa watu mbalimbali wakipokea adhabu ama thawabu kulingana na matendo yao. Mtume alipelekwa hadi Jehannamu ambapo anaona watu wakichomeka kwa moto mkali sana na kuzirai. Tukio hili ni dhihirisho kwamba jahanamu ipo kwa ajili ya watenda maovu. Kwa hivyo, linapaswa kuwaonya wale ambao hawajabadilisha mienendo yao. Umati wa Mtume unaonywa dhidi ya mbinu anazotumia shetani ili kuwaangamiza. Mwislamu hawezi kukataa tukio hili la *Ukawafi wa Miiraji*, kwa sababu limetajwa katika Kuran ambayo inaeleza kuwa Mungu aliumba mbingu saba na mtume Muhammad amepitia mbingu hizo zote. Katika kila mbingu tunaelezwa kuhusu mitume aliowapata. *Ukawafi wa Miiraji* ni mhimili/nguzo mojawapo kuu ya Kiislamu. mtume Muhammad alipewa sala tano

azilete kwa waumini. Kwa hivyo dhamira ya safari ya Muhammad ilikuwa ni kupata mawasiliano ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu hadi kwa waumini Waislamu.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumeangazia historia ya tenzi kwa ujumla na historia ya jamii ambamo wahusika katika tenzi hizi walichipuka. Tuliangazia mazingira na nyakati ambamo wahusika wa tenzi hizi walizaliwa. Aidha tulibainisha dhamira za watunzi wa tenzi hizi japo kwa ufupi mno. Katika sura hii tumeonyesha mazoea ya waandishi wa tenzi hasa katika kutanguliza na kutamatisha kazi zao. Hatimaye tumefafanua kisa katika *Ukawafi wa Miiraji* halikadhalika *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

# SURA YA TATU

# KUBAINISHA SIFA ZA WAHUSIKA NA MANDHARI KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* NA *UTENZI WAFUMO LIYONGO.*

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumebainisha sifa za wahusika katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Tungependa kuweka wazi hapa kuwa, tumeangazia uhalisiajabu katika tenzi, kwa hivyo tumewatenga baadhi ya wahusika ambao kwa maoni yetu, sifa zao hazitakuwa na mchango mkubwa katika kudhihirisha uhalisiajabu. Aidha tumeangazia umuhimu wa wahusika hao katika kukuza maudhui ya dini au ya kijamii.

Kulingana na TUKI (2004), wahusika ni viumbe waliosawiriwa au kubuniwa katika kazi ya fasihi ambapo wanaiga au kufanana na viumbe halisi duniani kwa kiasi fulani. Muhammad (1995), anaeleza kuwa wahusika ni viumbe vya mawazoni vinavyoumbwa na mwandishi na kuibuka katika kazi yake ya fasihi. Wahusika huhusika na matendo na matukio kadha katika kazi hiyo. Muhammad anaendelea kusema kuwa wahusika huweza kuwa viumbe vilivyochotwa katika maisha au uhalisia na pia huweza kuwa ni vivuli vya mawazoni, ambavyo havina mshabaha sana na maisha halisi duniani. Mwandishi huwaumba wahusika wake kutokana na mambo yafuatayo.

Tabia ya mtu fulani mwandishi anayempeleleza, huku akizidisha au kupunguza hiki na kile kwa mkono wake wa ubunaji kulingana na anavyotaka kumwasilisha au kumsisitiza. Tabia za mtu aliyemsikia akihadithiwa au aliyemsoma pahala, huku mwandishi akichukua nadhari ya makusudi kumbadilisha katika ubunaji wake ili awe amepunguka au amezidi kama anavyokusudia kumwasilisha. Dhana fulani kama vile za wema, ubaya, utu, ujahili, uadilifu, ugaidi na kadhalika, zilivyomvaa mwandishi na ambavyo anataka kuziwasilisha na kuzisisitiza kwa msomaji hujitokeza.

Muhammad (1995) anasema kuwa, kuna aina tatu kuu za wahusika; yaani wahusika mviringo, wahusika bapa na wahusika vinyago. Hivyo basi, wahusika wanatumiwa na msanii katika kuwasilisha kazi ya kifasihi. Wahusika huwa na sifa za kimaadili, kiitikadi, kitabia na kifalsafa, ambazo hutambuliwa kwa wanayosema na wanayotenda.Wahusika huchangia pakubwa katika uendelezaji wa maudhui na dhamira ya mwandishi. Njogu na Chimera (1999: 45) wanaeleza kuwa wahusika ni

sehemu ya fani, na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii.

Wahusika katika kazi ya fasihi hutegemeana ili kumfanya msanii afaulu katika kuwasilisha dhamira na maudhui yake. Mlacha (1989), anaeleza kuwa wahusika wapo huru, lakini pia wanategemea sana vipengele vingine vya fani. Wahusika hujengwa na vijisehemu vingi vilivyo huru, lakini ambavyo hutegemeana, na pia kila kimoja kinategemeana na kukamilishana, ili kumfanya mhusika awe kamili na aweze kuhusishwa na wahusika wengine pamoja na vipengele vingine.

Mdee (2011) anasema, mhusika ni mtu au mnyama katika hadithi anayetenda mambo kadha wa kadha kadiri mtunzi atakavyo ili kujenga hadithi yake. Kwa upande wake, Wamitila (2002) anasema kuwa wahusika ni viumbe wanaopatikana katika hadithi yoyote ile. Viumbe hawa huwa sehemu ya kazi nzima. Pili, wahusika ni binadamu wanaopatikana katika kazi ya kifasihi na ambao wana sifa za kimaadili, kitabia na falsafa ambazo hutambulishwa kwa wanayoyasema na wanayoyatenda. Maoni sawa na haya yanatolewa na Gatakaa (2012), anasema kuwa wahusika ni viumbe au watendi wanaotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira yake. Hutumiwa katika ujenzi na upelekaji mbele wa maudhui.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:45), wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii ambayo yaweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika ni viumbe wanaopatikana katika kazi ya kifasihi, wanaotambulishwa na mhusika au msimulizi na huwakilisha sifa tofauti zinazobainika kupitia kwa matendo yao.

Hivyo basi, wahusika huwa wa aina mbalimbali kama vile wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Wahusika wakuu ndio nguzo au ndio huchukua nafasi kubwa katika kuwasilisha lengo la msanii. Dhamira kuu ya mwandishi hujitokeza kupitia kwao na msimamo wa mwandishi kuhusu dhamira, matukio na vitushi vya hadithi hujibainisha kupitia kwa matendo na maneno yao. Mwandishi humkuza atakavyo, huku akimfanya atangamane na wahusika wengine kama vile wahusika wasaidizi. Wahusika wasaidizi hutumiwa kuwasaidia wahusika wakuu kujenga kazi na kusaidia katika kuupitisha ujumbe wa mwandishi. Wahusika

wajenzi wanasaidia kujenga wahusika wasaidizi na wakuu. Wao hawatokei sana kama wahusika wasaidizi au wakuu, bali husaidia kudokeza au kuongeza nguvu kwa masuala yanayoendelezwa na wahusika wakuu kwa usaidizi wa wahusika wasaidizi. Hii ndiyo maana Mlachi (1989) anaeleza kuwa wahusika wapo huru lakini pia wanategemeana .

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), kuna aina nyingi za wahusika kama vile mhusika mkwezwa, mhusika wa kimapinduzi, mhusika wa kisaikolojia na mhusika jumui. Mhusika mkwezwa ana sifa za kiutendaji anayetumia mantiki kufikia kauli na uamuzi lakini habadiliki licha ya mpito wa wakati. Mhusika wa kimapinduzi anaelewa historia, siasa, mazingira na hali ya jamii yake, na anajitolea kubadilisha maisha ya wanyonge. Mhusika wa kisaikolojia anakumbana na matatizo mengi ya kijamii na anaibusha hisia za huruma kwa msomaji. Mhusika jumui huwa ni mhusika mmoja mwenye sifa za wahusika wengi na anatumiwa kuonyesha fujo za maisha. Wamitila (2008), anaendelea kueleza kuwa wahusika wanaweza kuchunguzwa katika viwango vingine kama ifuatavyo:

Wahusika duara, ambao hubadilika kitabia, kimawazo na kisaikolojia na hubadilisha misimamo yao kulingana na mazingira.Wahusika bapa hawabadiliki kwa vyovyote vile, licha ya kubadilika kwa mazingira.Wahusika shinda ni wale ambao huonekana wasiokamilika. Wanatumiwa kuyakuza mawazo ya wengine, badala ya mambo yao wenyewe. Wahusika nguli ni wahusika wanaokamilisha maadili ambayo ndiyo aghalabu falsafa ya mwandishi. Mara nyingi, huwa ni mhusika mkuu anayetumiwa zaidi kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Mhusika wa kimapinduzi hutumiwa kuonyesha mapambano baina ya walio mamlakani, hasa viongozi wa kiimla na wanaopigania ukombozi. Tumeridhishwa na jinsi ambavyo wataalamu hawa wameangazia wahusika katika fasihi kwa hivyo, tunakubaliana na maoni yao na hivyo ndivyo tutakavyowatazama katika kazi yetu.

### 3.1 Wahusika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*

Katika utenzi huu, kuna wahusika binadamu tu. Wahusika hawa wanaweza kugawika katika makundi mawili: wahusika wenye sifa za uhalisiajabu na wahusika wenye sifa za kiuhalisia. Wahusika wenye sifa za binadamu wa kawaida ni kama vile: mamake Fumo Liyongo, kijakazi Saada, wanajamii na Sultani. Wahusika wenye sifa za

kushangaza ni kama Fumo Liyongo anayetenda matendo ya kuajabisha. Ana sifa za kiajabu ambazo si rahisi kwa mwanadamu wa kawaida kuwa nazo. Ana nguvu za sihiri, ana unene wa kimo, angeweza kupigana na jeshi la zaidi ya watu mia moja na sifa zingine ambazo tumeshataja. Kwa maoni yetu tunaonelea kuwa ni kupitia kwa matendo na sifa zake Liyongo ndipo uhalisiajabu unadhirika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

**3.1.1 Sifa za Fumo Liyongo.**

Mwandishi Kijumwa (1913), amemsawiri mhusika Fumo Liyongo kishujaa katika utendi wenyewe. Kwa upande wetu tumechukua mtazamo huo huo wa kishujaa alioutoa mwandishi ili kubaini sifa zake. Kwa mujibu wa Wamitila (2003), neno shujaa hutumika kueleza mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi ambaye anaweza kuwa wa kike au wa kiume. Kimsingi neno hili haliashirii wema tu. Kwa upande wake, Mulokozi (1979), anasema kuwa mashujaa wa utendi ni wa aina tatu: Mashujaa wa kijadi wa kiafrika kwa mfano, Fumo Liyongo katika *Utendi wa Fumo Liyongo,* mashujaa wa kidini kwa mfano, Mtume Muhammad na masahaba wake katika *Utendi wa Ras'lghuli* na mashujaa wa kubuni kwa mfano Tajiri mbaya katika *Utendi wa Masahibu.* Kutokana na ufafanuzi huu tumechunguza sifa za Fumo Liyongo kama shujaa wa kihistoria na zile za mtume Muhammad kama shujaa wa kidini. Kila jamii ina historia yake ambayo ni tofauti na jamii zingine. Kwa mfano, jamii ya Abagusii ina historia yao, jamii ya Wajaluo na jamii zingine. Vile vile historia hii huitofautisha jamii moja na nyingine. Kwa kauli hii, ni maoni yetu kwamba, mbali na madai ya Mulokozi, itakuwa vyema zaidi kumwangazia Fumo Liyongo kwa mawanda finyu kama shujaa wa jamii ya Waswahili. Aidha kwa sababu ya uwepo wa dini nyingi duniani kama: ukristu, uislamu, ubudha, ujuda, uhindu na zingine, ni msimamo wetu kwamba mawazo yetu yataeleweka vyema kwa kumwangazia mtume Muhammad kama shujaa wa dini ya Kiislamu. Katika kufanya hivyo tutakuwa tumeweka wazi dhamira yetu.

Mtunzi anamtaja Fumo Liyongo kama jitu nene, lenye kimo kirefu kinachozidi cha mtu wa kawaida. Kimo cha Fumo Liyongo kimeelezwa kwa kina, huku mtunzi akidhamiria kuweka wazi uwezo wa nguvu alizo nazo na umbo lake la kipekee. Alijulikana mno kwa unene wake kiasi cha kuwashangaza watu wengi. Watu walitoka mbali kuja kumtazama, kwani vimo vyao vilimfikia magotini:

Kimo kawa mtukufu,
Mpana sana mrefu ,
Majimbo kawa maarufu,
Watu huja kwangaliya, (ubeti wa 6)

Wagala wakipulika,
kwa dhihaka wakateta,
wakanena twamtaka,
na sisi kumwangaliya ( ubeti wa 16).

Mtunzi anaeleza alivyosafiri safari ya mbali kwa siku chache mno, hali ambayo ni tofauti na ya mwanadamu wa kawaida. Kwa mfano, aliwahi kutembea kutoka Shaka hadi jijini Pate , safari ya siku nne lakini yeye akachukua siku mbili tu na ya pili kwa hakika alikuwa anafika. Kwa hivyo hata haihesabiki.

Liyongo ni mwenye vipaji kadhaa: Anawashinda maadui katika kulenga shabaha anapotumia upinde na mishale kuchuma makoma bila kukwea mkomani. Juu ya yote alikuwa muungwana sana na mfano wa kuigwa na watu. Talanta inayojikeza hata zaidi ni, ufundi wa kutunga nyimbo na mashairi yaliyotumika katika ngoma ya *gungu*. Kwa mfano, akiwa kizuizini, aliitumia talanta hii kumtumia mamake ujumbe wa kisiri wa kishairi huku akiomba tupa ambayo aliitumia kukata minyororo ili kujipatia uhuru:

kamba Saada nakutuma,
enda kamwambie mama,
afanye mkate mwema,
kati tupa aitiya, (ubeti wa 104)

askari kuona,
ni wishwa wakatukana,
wa wishwa hula watwana,
mpekee haya ngiya (ubeti wa 108).

Liyongo alikuwa hodari katika vita, aliwashinda maadui wake wote hata Wagala walishindwa vita na Liyongo. Vimo vyao vilimfikia magotini hali hivyo ikawawia vigumu kumshinda vitani. Pia katika nguvu za kiakili, Liyongo alitumia akili kukataa kupanda mkomani ili aangue makoma:

Akawaambia "ngojani"
Akatowa mkomani,
Chembe kutia ngweni,
Makoma kuwanguliya (ubeti wa 65).

Ana nguvu za kimwili yaani ubabe na mabavu, kama inavyodhihirika katika beti zifuatazo:

Kimo kawa mtukufu:
Mpana sana mrefu,
Majimboni yu maarufu,
Watu huja kumwangalia, (ubeti wa 7)

Ni mwanamume swahihi,
Kama simba unazihi,
Usiku na asubuhi,
Kutembea ni mamoya (ubeti wa 13).

Ana nguvu za kiume na kidume. Wagalla walivutiwa na umbo la Fumo Liyongo kwa sababu ni mtu aliyekuwa na nguvu za kiume na wakamwomba Sultani wapate mbegu yake, jambo ambalo Liyongo alikubali. Sherehe ya ndoa ikaandaliwa , mtoto wa kiume akazaliwa. Liyongo akaishi Pate hadi pale ugomvi ulipozuka tena na Mringwari. Hili lilisababisha ahame Pate kuelekea msituni kwenda kuishi na Wasanye na Wadahalo:

Wagala wakabaini,
kumwambia sultani,
Twamtaka kwa thamani,
kijana kutuweleya,(ubeti wa 40)

Twaitaka mbegu yake,
Nasi kwetu tuipeke,
Kwa furaha tumeweka,
Apate kutuzaliya (ubeti wa 41)

Mke katukuwa mimba,
Akazaa mwana samba,
Mwanamume wa kutamba,
Mwana Liyongo sikiya (ubeti wa 46).

Alikuwa na nguvu za kiakili na kivita. Liyongo alikuwa na uwezo wa kiakili, kuvumbua mambo mbalimbali na nguvu za kivita alikuwa nazo.Vilevile sifa ya uganga na sihiri, Liyongo ana sifa ya uganga inayoonekana pale anasema hawezi kudhurika kwa njia ya kawaida inayomdhuru mwanadamu yeyote. Kile ambacho kingemdhuru yeye ilikuwa siri ambayo aliifichua kwa mwanawe. Yaani ni kwa kudungwa sindano ya shaba kitovuni:

Nisikiya wangu baba,
Liniualo ni haba,
Ni msumari wa shaba,
Kitovuni nikitiya (ubeti wa 143)

Liyongo ana mshikamano na kundi au makundi ya watu. Aliishi porini na Wasanye na Wadahalo na kushirikiana nao. Ni maoni yetu kuwa huenda ushirikiano huo ulimpelekea kufaidika kupata makao alipoenda kuishi mwituni nao. Liyongo anapokufa watu wengi waliompenda wanaomboleza kwa masikitiko makubwa:

> Make Liyongo hakika,
> Matanga aliyaweka,
> Watu wakasikitika,
> Kwa Liyongo kuifiya (ubeti wa 224).

Vilevile kulikuwa na ushirikiano wa kifamilia kati ya Liyongo na mamake, ushirikiano huu unamsaidia kutoroka gerezani baada ya mamake kumpelekea mkate wa wishwa uliotiwa tupa ndaniye:

> Mkate huu sikiya,
> Pishi mbili katimiya,
> Kati tupa katiya,
> Liyongo kampelekeya ( ubeti wa 107).
>
> Mama tupa katiya,
> Kitambaa metatiya,
> Kwa furaha mno ghaya,
> Sana kuwafurahiya (ubeti wa 110) .

Mbali na mhusika Fumo Liyongo, *Utenzi* wa *Fumo Liyongo* una wahusika wasaidizi, kama vile mfalme wa Pate, mwanawe Liyongo, wanajamii, mamake Liyongo, kijakazi Saada, Wasanye na Wadahalo. Hadhi yao ni ndogo, wamo utenzini kwa lengo la kumjenga mhusika mkuu. Wahusika hawa wana sifa za kihalisia ambazo kwa maoni yetu tulionelea kuwa hawana mchango mkubwa katika dhamira yetu tunayoitafiti- uhalisiajabu.

### 3.2 Sifa za wahusika katika *Ukawafi wa Miiraji*

Katika utenzi huu ni maoni yetu kuwa kuna aina mbili za wahusika: wahusika binadamu na wasiokuwa wa kibinadamu.Wahusika hawa wana sifa za ajabu. Wahusika hawa ni Allah, mitume, buraki, malaika na mke mwema. Kulingana na utenzi huu, Allah amesawiriwa kama mpeanaji. Yeye anampa Mtume nafasi ya kuomba anachotaka. Mtume anapoomba anapewa haja ya moyo wake. Allah anampatia Mtume sala mbazo atasali yeye na wafuasi wake wote. Kwa mujibu wa utendi, Allah anampa Mtume zawadi nyingi pia. Mhusika huyu anasawiriwa kama mwenye uwezo mkubwa usiokadirika.

### 3.2.1 Sifa za Allah

Inaaminika kuwa Allah ndiye aliyewahi kuishi mwanzoni mwa dunia kabla ya kitu chochote kuwepo duniani. Vyote vilivyomo ni kazi ya mikono yake. Inasadikika kuwa pasingekuwa na Allah, hapangekuwa na kitu au mtu duniani na mbinguni. Aidha inachukuliwa kuwa Allah ataendelea kudumu mbinguni na duniani siku zote bila kuwa na mwisho. Aidha mwisho na mwanzo wa Allah umepita fahamu za mwanadamu.

Allah ana mamlaka makuu kuliko kiumbe yeyote duniani. Inaaminika kuwa ana jeshi la malaika wengi mno, ambao amewapatia majukumu mbali mbali. Kwa mfano malaika Jibrili, Malik na wengine. Anaishi katika upeo wa juu kabisa zaidi wa mbingu ya saba ambapo ni vigumu kufika huko. Kwa Mujibu wa *Ukwafi wa Miiraji*, Mtume pekee ndiye alinafasika kuonana na Allah uso kwa uso.

Allah ndiye mwenye kuhukumu na kubariki. Kwa mujibu wa Kuran Tukufu, Allah atawaadhibu watenda maovu siku ya kiama ifikapo. Katika *Ukawafi wa Miiraji,* Allah amemweka malaika Malik katika lango la jahanamu yenye moto mkubwa unaoweza kuyeyusha hata mawe na vyuma. Moto huu upo kwa ajili ya kuwaadhibu watenda maovu na ibilisi siku ya kiama ifikapo. Kwa upande mwingine Allah atawazawadia wale watekelezao maamrisho yake wakati atakapoleta hukumu yake. Kwa mfano katika *Ukawafi wa Miiraji,* Allah amewatunuku mitume kama vile Ibrahim, Isa, Haruni, mtume Muhammad na wengine.

Allah ana uwezo mkubwa mno, ana uwezo wa kufanya kila kitu ambacho malaika na mwanadamu hawawezi kufanya. Kulingana na *Ukawafi wa Miiraji* aliziumba mbingu saba, akaumba ardhi na vyote vilivyomo. Amejijengea makao yake enzini ambapo si rahisi kufika huko ila watu wateule tu kama mtume Muhammad ndio wapatao nafasi ya kuonana na Allah ana kwa ana kama Mtume alivyoenda kupokezwa sala.

Allah anaaminika kuwa na umbo la ajabu tena la kipekee. Hakuna anayeweza kudai kuzifahamu sifa za Allah kikamilifu, hata mtume Muhammad hakuweza kueleza sifa za Allah kikamilifu. Kwa mujibu wa *Ukawafi wa Miiraji* aliyoyaona Mtume, hakuna mdomo unaoweza kuyaeleza aidha yalikuwa ng'ambo ya mawazo ya mwanadamu. Haiwezekani mtukufu awe ni mwenye kusifika kwa sifa sawia na za kusifia viumbe

au vitu, kama vile: kuwa na rangi, kusimama, kukaa kitako, kupanda juu, kushuka chini, kulala, kuamka, kusahau, kughafilika, na mifano ya sifa kama hizo. Aidha haiwezekani Allah mtukufu kusifika kwa chochote kwa kutaja sifa za viungo, kama vile kuwa na uso, jicho, pua, sikio, mkono, mguu, na sehemu za mwili kama hizo. Pia haiwezekani kuwa yeye amejihusisha na sehemu au mwelekeo wa upande fulani au wakati fulani, au ukaribu na umbali wa masafa. Sifa ya upekee wa Allah inabainika zaidi hata katika Biblia takatifu:

> Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu chochote,
> kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani,
> wala kilicho majini chini ya dunia
> ( kutoka 20:2).

### 3.2.2 Sifa za mtume Muhammad

Kwa mujibu wa *Ukawafi wa Miiraji,* Muhammad ndiye aliyeenda mbinguni na kurudi ardhini kwa kutumia "Miiraji' ambayo ni ngazi ya kupandia mbingu. Mhusika Muhammad ana sifa za kutajika kuanzia wakati anapotakaswa hadi anapopokezwa sala kutoka mbinguni. Mtume Muhammad amesawiriwa kama mhusika mteule. Ameteuliwa kwa sifa njema ya uaminifu, anajiwa na malaika Jibrili, Mikaili na malaika mwingine ambao wanamwamsha Mtume. Jibrili anamhakikishia mtume Muhammad kwamba Mungu anamwita, hivyo ilimbidi asalishe sala (ubeti wa 4). Katika Kuran Tukufu, kuna aya inayompa sifa mtume Mohammad kwa unyenyekevu wake na kumweka katika wadhifa mkuu. Kuna baadhi ya hadithi pia zinazozungumzia suala hili na kudhihirisha umuhimu wake mkubwa katika dini ya Kiislamu. Mtume Mohammad amewekwa katika daraja ya juu kutokana na hulka na mienendo yake iliyomfanya kuweza kuaminika. Yeye alikuwa akitimiza ahadi zote alizotoa kwa wakati unaotakiwa. Hakukengeuka kitabia wala kupoteza uaminifu aliokuwa nao. Hakuweza kusema uongo hata kwa dhihaka. Mtume Mohammad amekuwa mfano bora kwa Waislamu kutokana na hulka yake, tabia yake, huruma, unyenyekevu, mwenye kutabasamu na mpole. Hakuwa na moyo wa chuki wala roho mbaya. Kinywa chake hakikuwahi kutoa maneno wala kauli chafu inayoweza kuvunja mtu moyo. Hakuwahi kutoa aibu ya mtu mbele ya hadhira bali alikuwa mpole mwenye utulivu na subira.

Alikuwa akiwasamehe waliomkosea na hakuwekea mtu yeyote chuki wala husuda. Kila alipoalikwa, alijitahidi kadri ya uwezo wake ili kuhudhuria. Hakuvunja mtu

moyo na alihimiza usawa katika jamii pasi na kuzingatia tofauti za utajiri au umasikini, ubwana au utumwa, ukubwa au udogo. Alihimiza misaada kwa watu maskini, kutembelea wagonjwa na kutazama mayatima. Anas ambaye alimhudumia mtume Mohammad tangu alipokuwa na umri wa miaka kumi, pia amemsifia kwa kusema kwamba hakuwahi kumsikia akimkemea wala kumkasirikia kwa jambo lolote katika maisha yake.

Mtume Muhammad pia alitoa mafunzo ya utekelezaji wa ibada za Mwenyezi Mungu kwa umma wake wa Kiislamu. Alisisitiza umuhimu wa kutekeleza ibada hizo mara kwa mara pasi na mapungufu. Aliwaeleza watu kuwa wanadamu wameumbwa kwa lengo la kumuadubu Mwenyezi Mungu pekee. Vile vile ametuhusia kuwa ibada na matendo mema ya misingi ya kidini ndiyo yanayoimarisha imani ya mwanadamu. Mtume Mohammad pia aliwapigania Waislamu ili kurahisishiwa ibada za Mwenyezi Mungu. Kwa mfano, waliruhusiwa kufupisha ibada za swala hasa wanapokuwepo watoto, kina mama na wazee katika safu za maamuma.

Tangu udogo wake Mtume aliondokea kuwa na sifa nzuri ambazo hapana hata mmoja katika hirimu zake aliyekuwa nazo zote. Kila sifa zinazohesabiwa kuwa ni njema na Waislamu ndizo alizokuwa nazo tangu utoto wake. Mkewe (Aisha) alipoombwa kutaja kidogo sifa za Mtume, alisema hivi: "Sifa zake ni zile sifa nzuri zinazosifiwa na kuran" na katika Kuran zimetajwa chungu ya sifa zilizo nzuri. (Sura: 19: 10-15)

Mtume mara nyingi alikuwa akisema: "Sikupata kufanya hata siku moja yale mambo waliyokuwa wakiyafanya makafiri." Kwa hivyo yeye hakupata kuabudu sanamu, kulewa, kuzini, kucheza kamari wala hakumdhulumu mtu kitu chake na mengine kama hayo. Lakini alikuwa msema kweli, mwaminifu, mpole na mwenye haya na sifa nyingi nyinginezo bora kama hizi. Watu wa Makkah walikuwa wakimsifu kwa tabia zake, hata wakampa jina la Muhammad Al-Amin (mwaminifu).

**Umuhimu wa mtume Muhammad**

Mtume Muhammad ametumiwa kudhihirisha utukufu wa Mungu kwani Mungu hapendezwi na nyoyo chafu, ndiposa Mtume alipasuliwa na kutakaswa. Mtume ametumiwa pia kuonyesha uhusiano wa Mungu na binadanu, hasa Mtume anapopelekwa hadi mbinguni na hatimaye kurejeshwa ardhini. Tukio hili ni

dhihirisho kuwa hata leo, Mungu anawaita baadhi ya watu (manabii) ambao anawasiliana nao moja kwa moja. Matukio yanayomkumba Mtume ni dhihirisho la nguvu za Mwenyezi Mungu. Kutokana na sifa tele za mtume Muhammad, tunatoa rai kuwa, yeye ametumiwa kama mwongozo bora kwa waumini wote wa Kiislamu. Jukumu lake kuu ni kuwa kielelezo au mfano bora wa kuigwa na kila muumini. Mtume ndiye mvumbuzi, mwanzilishi wa dini ya kiislamu. Pasipo yeye hapangekuwa na dini tukufu ya Kiislamu kwa hivyo ni kupitia kwake ndipo dini hii ikachipuka. Ni maoni yetu kuwa maandishi takribani yote katika Kuran na hadithi za Kiislamu zipo kutokana na uwepo wa mtume Muhammad.

### 3.2.3 Sifa za Walinzi / Mitume wa mbingu saba

Kwa mujibu wa *Ukawafi wa Miiraji*, mitume wanachangia sana katika imani ya dini kwani ni katika imani tu ndio mambo ya kimbingu huaminika. Aidha utenzi huu unadokeza kuwa asiyekuwa na imani basi hauna neno naye (dibaji). Ni katika imani ndio wanatoa uthibitisho kwamba kweli mtume Muhammad alipanda kwenda mbinguni kwani hata mitume walishaenda katika mbingu hiyo hiyo. kwa mfano Enokhu alitembea na Mungu (mwanzo 5:24) kwenda mbinguni bila kupitia kwa mauti. Mfalme wa pili, Elijah alichukuliwa mbinguni kwa gari la moto na upepo wa kisulisuli. Kwa hivyo alienda mbinguni akiwa hai bila kuhisi uchungu wa mauti. Mtunzi ananukuu kufufuka kwa Isa toka kwa wafu huku akipokelewa mbinguni na kukaa katika mkono wa kuume wa baba (Mariko 14:62). Tunatoa rai kwamba mitume wametumiwa kama vielelezo kamili vya kuigwa na waumini wa dini ya Kiislamu kwani wao ni binadamu lakini walijibidiisha hadi kuukaribia utakatifu wa Allah. Hivyo wanawamotisha waumini kuwa hata wao wakitii amri za Allah, basi wanaweza kufika mbinguni jinsi walivyofika.

**Umuhimu wa mitume /walinzi wa mbingu saba.**

Mitume hawa ni dhihirisho kuwa katika maisha ya sasa, Mungu huwateua watu wake ambao anawatwika kusimamia binadamu, kama vile, wasimamizi wa kanisa, vyuo vya elimu na sekta nyinginezo. Mungu ana mamlaka ya kuchagua awapendao, na kuwapa majukumu yampendezayo.

### 3.2.4 Sifa za Malaika.

Ni viumbe wa mbinguni ambao Allah huwatumia apendavyo katika kutekeleza shughuli zake. Katika *Ukawafi wa Miiraji*, kila malaika ana majukumu yake maalum kama alivyopewa naye Allah. Kwa mfano malaika Jibrili ndiye aliyepasua kifua cha Mtume, akakitakasa hadi kikatakasika kisha anakishona upya. Jiburili ndiye aliyemhimiza Mtume kufanya sala mara kwa mara. Aidha Jiburili alimtolea Mtume fasiri ya matukio mbali mbali waliyokumbana nayo wakiwa safarini. Yeye ndiye aliyemwongoza Mtume kuanzia mwanzo hadi alipomfikisha katika mbingu ya saba. Kwa upande wake Mikaili, yeye alidhihirika akitumwa katika kuleta na kupeleka hiki au kile. Kwa mfano yeye ndiye aliyeleta maji yaliyotumiwa kumwoshea Mtume, kisha akaleta tena kifaa cha dhahabu.

Pia kuna malaika aliyeitwa Malik, yeye hana furaha. Ni malaika wa kuzimuni, hulinda lango la moto mkubwa wa ahera. Hufunga na kufungua lango la ahera kwa amri yake Jibrili. Tunakisia kwamba, malaika huwa kama daraja kati ya mbinguni na duniani au kati ya Allah na wanadamu. Mbali na kudhihirisha ukuu wa Allah, wahusika malaika wanathibitisha mpangilio maalum uliopo mbinguni kwani kila malaika ana wajibu wake. Wahusika hawa pia wanatoa mchango mkubwa katika kujenga maudhui ya dini ya kiislamu hasa katika kuwaonya watenda maovu:

> Kisha wakaona watu wawi wakila nyama,
> Mbiti wakiwata nyama mbivu ilio ngema
> Jiburilu kamba : ni wazinzi walipokoma
> Wake na waume wazingao wasiokoma (ubeti wa 20).

### 3.2.5 Sifa za mke mwema

Jibrili na mtume Muhammad walienda wakamwona mke mwema ambaye alinukia harufu nzuri iliyopendeza (ubeti wa 15). Alikuwa msusi, hivyo basi alikuwa anamchana nywele ya mke mwasi asiyekuwa na huruma. Mke mwema pamoja na watoto wake walitumbukizwa kwenye mafuta yaliyochemka, na harufu nzuri ya kupendeza ilinukia kwenye makaburi yao.

**Umuhimu wa mke mwema.**

Harufu nzuri ya kupendeza iliyonukia baada ya mke mwema na watoto wake kutumbukuzwa kwenye mafuta yaliyochemka ni dhihirisho kuwa duniani kuna watu

wema wanaompendeza Mungu. Mwanamke mwasi asiye na huruma anawakilisha watu wabaya na wasio na utu duniani.

### 3.2.6 Sifa za watu waovu

Jibrili na mtume Muhammad waliwaona watu waovu ambao wanapiga vichwa vyao kwa nyundo za chuma. Malaika alimwelezea kuwa hawa walikuwa watu waovu ambao hawakupata wakati wa kusali, hawakutoa zaka na waliopuuza sala. Jibrili na mtume Muhammad wanawaona watu waovu wanaovalia matambara, ambao kamwe hawakutoa zaka, ili kuwasaidia wasiojiweza. Mtume anawaona wazinzi au waasherati walioshiriki ngono nje ya ndoa na pia aliona mtu aliyekuwa njiani ambaye anararua nguo za watu wanaopita njiani. Jibrili anamweleza Mtume kuwa hatima ya watu hao ni jahanamu:

> Kisha wakenenda wakaona watu dhamamina,
> Jibrili kwamba: watu zao si watu wema,
> Wakipondaponda vitwa vyao nyundo za chuma,
> Hawatoi zaka, mali yao ya Jehannama (ubeti wa 18)

**Umuhimu wa watu waovu.**

Watu waovu ni kiwakilishi cha binadamu waovu katika maisha ya kawaida. Wao hawana huruma, hasa kwa wasiojiweza. Hatima yao ni jahanamu, ambako watasumbuka milele. Vile vile wazinzi au waasherati wanawakilisha makahaba na waasherati waishio duniani leo. Wao huharibu ndoa zao, na hasa kusambaza virusi kama vile vya ukimwi, ambalo ni janga la kitaifa. Mti uliopo njiani unaorarua nguo za wapita njia ni kielelezo cha watu waovu wanaokaa barabarani kuwangoja wapitao, ili wawadhulumu kwa kuwakosesha amani. Hatima ya uovu wao ni jahanamu pia.

### 3.2.7 Sifa za buraki

Ni mnyama ambaye alimbeba Mtume katika kupanda hadi mbingu ya saba. Ni mweupe, ambaye ni mkubwa kuliko punda lakini mdogo kuliko farasi. Alipokwea mlima, miguu yake ya nyuma hurefuka. Alipoenda kwenye bonde au mteremko miguu ya mbele hurefuka. Ni mtiifu kwa malaika Jibrili na kwa Muhammad kwani alifuata maagizo yote anavyoelekezwa hatua kwa hatua hadi mbingu ya saba: Alimbeba Mtume kwa amri ya Malaika Jibril, alitua na kuondoka katika kila mbingu alipoelekezwa kufanya hivyo. Ana mbawa mbili, amejawa na ushupavu. Alitembeza

kwato zake umbali sawia na ndoto/maono aliyoyaona Mtume ndiye aliyempeleka Mtume na kumrejesha toka mbingu ya saba.

**Umuhimu wa buraki**

Ni maoni yetu kuwa mhusika huyu, anatoa nafasi muhimu ya kudhihirisha utukufu wa Allah. Allah ana uwezo wa kutumia kiumbe yeyote atakaye katika kutelezea matakwa yake. Aidha kupitia buraki upekee au usipesheli wa Mtume unaonekana. Kwa mujibu wa utenzi ni yeye tu aliyewahi kubebwa na mnyama wa aina hiyo. Isitoshe upekee huo ni kigezo muhimu katika kukuza mvuto kwa Waislamu, hivyo kukuza imani ya waumini hata zaidi. Buraki ametumiwa kuonyesha baadhi ya wanyama ambao wana usaidizi mkubwa katika maisha ya binadamu kama vile punda, ngamia, ng'ombe na wengineo. Hata hivyo, kuna wanyama wengine ambao ni tisho kubwa kwa binadamu kama vile nyoka, simba na chui. Wanyama hawa huhatarisha maisha ya binadamu.

Wahusika hawa wa mbinguni ni wa ajabu. Katika *Ukawafi wa Miiraji* wao wanawezesha yasiowezekana katika ulimwengu wa kawaida kufanyika. Kwa mfano wao ndio wanaomleta buraki ambaye anambeba Mtume kwa safari ya mbingu saba. Wahusika hawa wanawezesha matukio yote ya kiajabu kutendeka ambao katika hali halisi hayawezekani kutendeka. Ni mtazamo wetu kuwa pasi na wahusika hao wa kifantasia, kusingekuwa na uhalisiajabu katika *Ukwafi wa Miiraji.*

## 3.3 Sifa za Mandhari

Wamitila (2008) anasema kwamba mandhari ni mazingira ya kimahali, kiwakati na ya kihistoria ambamo kazi fulani ya kifasihi inajikita. Tunaunga mkono mawazo haya, kwa hivyo tunachukua mtazamo wake katika kuangazia sifa za kiuhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

### 3.3.1 Mandhari ya kisimani

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, mhusika Liyongo alipochomwa sindano ya shaba kitovuni, alizinduka usingizini, akabeba uta na mishale kuelekea kisimani. Alipofika huko, akapiga goti huku akilenga mshale kuelekea mjini. Mazingira ya kisimani yalisalia mahame, watu wakawa hawaendi huko kuchota maji. Ni vigumu, kujua ni kipi kilichomsababisha Liyongo kukaa kisimani kwa muda mrefu. Wanakijiji

walikosa maji kwa sababu, kisimani palikuwa panatisha. Walijawa hofu ya kushambuliwa na Liyongo.Watu waliteseka kwa kukosa maji siku kadhaa hadi ikawabidi kumuomba mamake aende ambembeleze. Alipofika kisimani, aligundua kuwa Liyongo alikuwa mfu.

### 3.3.2 Mandhari ya mbinguni

Katika *Ukawafi wa Miiraji*, tunakisia kuwa mazingira ya mbingu ya kwanza hadi ya sita huenda yanashangaza na kuogofya. Mazingira ya mbingu ya saba ndiyo yamefafanuliwa zaidi jinsi yalivyoogofya. Katika mbingu hiyo pamejaa mwanga wa nuru na kudura ya Allah. Sifa ya mbingu hii hakuna mdomo unaoweza kueleza. Mtume akiwa katika hali ya mshangao alivutiwa na mmea ulioitwa Sarat ambao ulinawiri vyema kwa upande wa kulia mwa kiti cha enzi cha Allah. Matawi yake yalisambaa zaidi ya umbali wa kati ya jua na ardhi.

Malaika walikuwa wengi zaidi ya mchanga wa pwani. Malaika hao wanafurahi chini ya kivuli cha mti huo, wote wakiwa wanasoma aya za Kuran Tukufu. Majani ya mti huo ni sawa na masikio ya tembo, matunda yake yalikuwa makubwa kama mitungi, matunda hayo yalikuwa matamu na meupe kuliko maziwa. Mti huu ulipogubikwa na amri za Allah, ulibadilika na kuwa katika hali ambayo hakuna kiumbe aliyeweza kuufananisha kwa uzuri wake. Kulikuwa na mito minne karibu na mti huo: miwili ikiwa haionekani na miwili ikiwa wazi yaonekana. Mtume Muhammad aliongozana na Jibrili hadi nyumba ya kusujudia, iliyokuwa na sifa za kupendeza sana. Nyumba ilijengwa na mawe sita ya njano. Walifika mahali ambapo Jibril hawezi kusonga mbele kwani hapo ndipo palikuwa kikomo chake. Muhammad anaendelea peke yake, mwepesi hata kuliko mawazo, alipitia katika uwanja mkubwa uliogawika mara mbili; eneo moja la uwanja huo liliwaka taa na lingine lilijaa giza tupu. Akazidiwa na woga na ukimya kwa sababu ya kuwa pweke. Mara hiyo alijiwa na wimbi la furaha, yaliyofuatia ni manukato mazuri yaliyonuswa na Mtume pekee.

### 3.3.3 Mandhari ya jahanamu

Malaika Jibrili akamwonyesha Mtume moto mkali,akaona adhabu kali zilizokuwa zikitolewa hadi Mtume akashindwa kustahamili akapigwa na mshangao hadi akazirai. Jibrili akamkumbatia ndipo fahamu zikamrudia.

**Umuhimu**

Mandhari haya yanatoa onyo kali, kwa watenda dhambi kuwa wanafaa kukoma kutenda dhambi la sivyo adhabu kali ya moto inawangojea. Aidha ukuu wa malaika unadhihirika kwani yeye hakudhurika kwa moto. Malaika ndiye anayemkumbatia Mtume anapozimia dhidi ya makali ya moto.

**Hitimisho**

Sura hii imehusu sifa za wahusika ambao kwa maoni yetu wanadhihirisha uhalisiajabu. Katika *Ukwafi wa Miiraji* tulibaini kuwa takribani wahusika wote wana sifa za kushangaza hali ambayo ni tofauti katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* wenye mhusika mmoja wa kiuhalisiajabu. Pia tumegundua kuwa, kuna wahusika wenye sfa za kibinadamu na wasio na sifa za kibinadamu. Aidha tuliangazia wahusika wanyama pamoja na mandhari yenye sifa za uhalisiajabu.

## SURA YA NNE

## SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA *UTENZI WA FUMO LIYONGO* NA *UKAWAFI WA MIIRAJI.*

### 4.0 Utangulizi

Katika sura ya tatu tumezunguzia sifa za baadhi ya wahusika ambao kwa maoni yetu wana sifa za kushangaza. Tulifanya hivyo kwa misingi kuwa wahusika hao, ndio waliosheheni sifa za kiuhalisiajabu. Katika sura hii, tumeshughulikia sifa za kihuhalisiajabu zinazobainika katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji.* Sifa za kiuhalisiajabu tulizozishughulikia ni pamoja na:- kuwepo kwa wahusika ambao si wa kawaida, matukio ya kiajabu, kuvunjwa kwa mipaka ya mahali pa kufanyika vitendo. Sifa nyingine ya kiuhalisiajabu ni kule kuwepo kwa hali za kushangaza na za kuogofya. Katika uhalisiajabu huwepo wakati ambao ni wa kistari na wa kiduara. Katika kazi ya kifasihi huwepo matukio ya kindoto au ya kifantasia. Mara nyingi wakati wa kazi ya uhalisiajabu hausongi. Mpaka kati ya yanayowezekana, mambo halisia na yasiyowezekana unafutwa au haupo.

### 4.1 Matukio yanayoogofya na yanayoshangaza.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* kuna matukio ya kiajabu ambayo yameibuka kama njia moja ya kuendeleza utenzi huu. Haya matukio ya kiajabu ni kama vile sifa za unene usio wa kawaida ambazo mtunzi amemmiminia Fumo Liyongo. Sifa alizopewa Fumo Liyongo zinamwacha msomaji wa utenzi huu na mshangao mkubwa huku akijiuliza kama kweli Liyongo ni binadamu, jitu au ni kiungu fulani. Kwa mfano, mwandishi anasema kuwa Liyongo angeweza kutembea kutoka Shaka hadi Pate safari ya mbali kwa siku mbili tu, ilihali binadamu wa kawaida angechukua siku nne. Liyongo anadai kuwa hangeuawa kwa kupigwa mkuki ila kwa kudungwa sindano ya shaba kitovuni mwake, hata anapouawa anabakia kisimani akiwa amepiga magoti huku amewatisha watu wengi bila wao kujua kuwa alikuwa ameshaaga dunia.

Wagalla walijawa na hamu kubwa ya kutaka kumwona Liyongo, hivyo walimwambia Sultani ambaye alimwandikia barua ya wito. Liyongo anaandaa safari ya kutoka Shaka hadi Pate. Anapofika jijini Pate anapuliza panda ya kwanza ilipasuka. Panda ya pili nayo haikustahamili, vile vile ilipasuka. Watu wakashangaa mno hadi

wakaulizana ni nini kimetokea. Sultani akawaeleza kuwa ni Liyongo amewasili. Liyongo kupuliza panda hadi kupasuka ni tukio la kuogofya na kushangaza pia. Si jambo la kawaida mtu kupuuliza panda hadi kutostahamili pumzi zake. Isitoshe, si panda moja, alipuliza mbili moja baada ya nyingine wakati huo huo mmoja. Aidha panda yenyewe ilitoa sauti ya juu inayotisha ambayo si ya kawaida kiasi cha watu kushangaa na kutaka kujua ni jambo gani la mno limetokea.

Liyongo alipofika Pate alitua mkoba aliokuwa amebeba. Kwa mujibu wa utendi vitu alokuwa amebeba vingetosha kujaa nyumba nzima. Watu/Wagalla wanapoona vitu alivyokuwa amevibeba wanashangaa na kujawa na woga. Kwa kawaida, haiwezekani mwanadamu kubeba mizigo iwezayo kujaa nyumba yote, ajabu ni kwamba Liyongo anabeba vitu hivyo kisha akasafiri hadi Pate.

Watu wa ukoo wa Sultani ambao walikuwa wakuu wa vita, walimwogopa sana Liyongo katika vita. Mara tu wanapomwona Liyongo, walijawa hofu. Kwa mujibu wa utenzi wengine walitoa mkojo kwa woga uliowaingia walipomwona Liyongo. Hivyo hawakuweza kupigana naye kwani alikuwa na uwezo wa kuwapiga wapiganaji wa vita wanaume zaidi ya mia moja. Katika hali ya kawaida haiwezekani mtu mmoja kuwatisha wengine hadi kujikojolea au kuwashinda wapiganaji mia moja kiasi cha wao kutorokea usalama wao. Liyongo kuogofya na kuwa na uwezo mkubwa wa kivita wa kuwatorosha watu zaidi ya mia moja ni tukio la kiajabu.

Sultani alijaribu kwa mbinu kadha kumwangamiza Liyongo, nyingi za mbinu zake hazikufua dafu. Akabaki amesinywa ni kwa namna gani angeweza kumwangamiza Fumo Liyongo. Katika jaribio lake la mwisho alimwahidi mwanawe Liyongo ahadi chungu nzima ikiwa angegundua kile kiwezacho kumdhuru babake. Katika kubaini haya, Liyongo anajiwa na mwanaye ambaye anamweleza kuwa hawezi kudhurika wala kuuliwa kwa silaha yoyote ila kwa sindano ya shaba ikitiwa kitovuni mwake. Kwa mujibu wa utenzi wenyewe, hili ndilo tendo la pekee litakalomuua Liyongo. Katika maisha ya mwanadamu wa kawaida, haiwezikani kutouliwa au kutodhurika kwa silaha zingine. Ukweli ni kwamba silaha yoyote inaweza kusababisha maafa au maumivu kwa mwili wa mwanadamu. Huu ni mfano wa tukio la kushangaza na kuogofya katika utendi huu.

Fumo Liyongo alikuwa na uwezo wa kutambua mawazo yaliyomo akilini mwa watu, kujua yale matukio yakayotokea, yatakayowapata watu au yale ambayo yangempata baadaye. Kwa mfano alijua kuwa mwanawe amedanganywa kwa kupewa zawadi ili aje kumsaliti. Liyongo alimwonya kwa hili na akamwambia kuwa maisha yake yatamharibikia. Mbali na mwanawe kukataa ukweli huo kata kata, kulingana na utenzi ni kweli kuwa hivyo ndivyo hali ilivyokuja kumtendekea. Alisalitiwa na jamii yake jinsi alivyomsaliti babake na kufukuzwa aende mbali na mji. Ahadi alizopewa za kuozwa bintiye Daudi Mringwari hakutelezewa. Hatimaye anaugua ugonjwa wa ajabu usiokuwa na tiba. Matukio haya katika utendi ni ya kuogofya na kushangaza.

Wasanye na Wadahalo walipomdanganya kuwa wao ni marafiki kwa hivyo aupande mkoma, Liyongo aligundua mbinu hii na kuwadanganya kuwa yeye ni maskini na hataweza kulisha kikoa. Tamaa yao ilikuwa akiukwea mkoma wamfume mishale. Aligundua uwongo huo kwa hivyo akaliangusha tawi zima la makoma kwa kulifuma mshale bila kukwea mkomani. Isitoshe akiwa bado anaishi Pate Sultani anapanga njama ya kumwangamiza, lakini Liyongo anatambua njama hii hivyo anapahama Pate na kukimbilia mwituni. Uwezo huu wa kutambua mipango ya watu/mtu iliyomo akilini ni sifa ya kushangaza na kuogofya.

Liyongo ana kimo kikubwa cha ajabu; ni mnene, pandikizi la mtu. Kwa mujibu wa utenzi Wagalla walimfikia magotini. Walipomwangalia walikubali kuwa ni mtu mrefu kweli. Wagalla wanatamani sana mbegu yake, kumwomba awaolee msichana wao. Kimo cha Liyongo ni muujiza wa aina yake kwa sababu Wagalla wanashangaa kuona alivyokuwa mrefu. Katika dunia halisi hapajakuwa na mtu mwenye ukubwa wa Liyongo. Tambo la mwili alilokuwa nalo Liyongo ni la kushangaza na kuogofya mno.

Kifo cha Liyongo ni muujiza mtupu. Alichukua uta na mshale na kuondoka mbio mbio kuelekea kisimani, huku akimtafuta muuaji. Alipofika karibu na kisima, analenga mshale tayari kuufuma. Watu wengi walipoona, wanatorokea mbali hata hawakukaribia kisimani. Watu walitaabika kwa kukosa maji kwani waliogopa kwenda kisimani alipofia Liyongo. Katika hali ya kawaida haiwezekani mtu awe amefariki na aweze kupiga goti, ashike upinde na mshale, kisha asimame wima kwa goti asianguke na awatishe watu walio hai.

Liyongo alifaulu kukereza minyororo, kwa tupa kiasi ya askari kutosikia au kubaini si jambo la kawaida. Isitoshe baada ya kuikata minyororo watu wengi walikimbilia usalama wao wakiwemo askari walinzi wa gereza. Alitembea huru huria kutoka kwenye kituo cha askari hadi anafika barabarani. Liyongo ana sifa ya kucheza ngoma ambayo ni ya kipekee, ilikuwa na umaarufu usiokuwa wa kawaida.

### 4.2 Matukio ambayo yanaogofya na kushangaza katika *Ukawafi wa Miiraji.*

Malaika waliomjia Mtume hawakupitia mlangoni, walimjia Mtume kwa namna ya ajabu kwa kupitia paani. Haieleweki jinsi walivyoweza kupitia hapo na kumjia Mtume. Aidha haifahamiki ikiwa walivunja paa au hawakulivunja. Haiwezekani kwa binadamu wa kawaida kuingia paani bila kubomoa kwa kutumia vifaa maalumu. Lakini kwa muda mfupi kabisa, malaika wanamjia Mtume na kumwamsha mara ya kwanza, mara ya pili na mara ya tatu.

Kuna masafa marefu yasiyokadirika kati ya dunia na mbingu. Kwa sababu ya umbali uliopo, inaaminika kuwa itachukua muda mwingi sana ili kuifikia mbingu. La kushangaza ni kwamba Mtume anasafiri hadi mbingu ya saba na kurudi kwa usiku mmoja tu. Katika maisha ya kawaida haiwezekani mtu yeyote kuwa na uwezo wa kwenda mbinguni wala hatujapata ushahidi wa mwanadamu aliyewahi kwenda mbingu ya kwanza hadi ya saba. Aidha haiwezekani mtu kusafiri kwa usiku mmoja tu.

Mtume Muhammad alisafiri kwa mnyama anayefanana na farasi lakini mwenye mbawa. Kwa mujibu wa utendi, mnyama huyo ndiye aliyembeba Mtume na alikuwa na uwezo wa kupanda hadi mbinguni kwa kasi ajabu. Ni mnyama spesheli ambaye ni Mtume tu aliyewahi kumtumia katika kupanda kipandio cha kuelekea mbinguni. Katika maisha halisi, hatujapata ushahidi wa kuwepo kwa mnyama wa ajabu mwenye maumbile kama ya buraki.

Mtume alipasuliwa kifua na malaika, akatakaswa kisha akashonwa. Kulingana na *Ukawafi Wa Miiraji* hapakuwa na alama yoyote iliyosalia ya kuonyesha kuwa pengine Mtume amekatwa au kushonwa. Hatimaye alitiwa muhuri wa utume halafu akaonyeshwa mnyama buraki ambaye anaambiwa ampande tayari kwa safari. Hali ya Mtume kupasuliwa kifua na kushonwa mara hiyo hiyo na jeraha kupona bila alama

yeyote kuonekana ni tukio la ajabu. Aidha Mtume anakuwa na ujasiri wa kumpanda buraki tayari kwa safari.

Tukio lingine la kiajabu ni pale ambapo Mtume alipita katika mbingu zote katika kila mbingu alikutana na manabii tofauti tofauti. Safarini aliona matukio mbalimbali ya kushtusha ambayo malaika Jibrili anampa fasiri yao. Kwa mfano, waliona mto wa damu na ndaniye mlikuwamo watu. Waliwaona watu mbalimbali, kuna wale waliokatwa ndimi zao kwa makasi kisha zikaota wakati huo huo. Pia waliona watu waliojikwaruza nyuso zao kwa kucha, wakaona watu waliokuwa wanakula nyama mbichi na kuiacha iliyopikika vyema. Mtume na jibrili waliona matukio mengi ya kuogofya wakiwa safarini huku Malaika Jibrili akimfasiria Mtume maana zao na ni kwa nini hayo yalitokea.

Mtume kushuhudia jahanam ni tukio la kushangaza. Jibrili na Mtume wakiwa safarini walikutana na Malik ambaye ni bawabu wa peponi. Kisha Jibrili alimwambia Malik afungue lango la jahanam. Alipolifungua, Mtume aliona moto mkubwa na mkali ulioweza kuyeyusha hata mawe. Alionyeshwa adhabu kali wapewayo watu hadi Mtume akashindwa kuhimili. Kutokana na makali ya moto huo, Mtume alipoteza fahamu ndipo malaika alipomwauni.

Pia Mtume alionyeshwa peponi ambapo mfanowe hajawahi kuona tena. Peponi palipambwa kwa fedha na dhahabu nyingi anuwai. Hatimaye Mtume anaenda juu zaidi ya mbingu saba hadi mahali kunakozidi fahamu za binadamu. Hili ni tukio la kushangaza kwa namna ya kipekee. Mtume anaendelea na safari hadi kipeo cha juu ambapo hata malaika Jibrili hakuruhusiwa kufika huko.

Matukio haya ya kushangaza yameshamiri mno katika *Ukawafi wa Miiraji*. Mtume alipata nafasi ya kipekee ya kuonana uso kwa uso na Allah. Aidha walifanya mazungumzo ambapo Mtume anapewa sala hamsini kwa ajili ya umma wake. Alienda kwa Mtume Musa ambaye alimshauri arejee kwa Allah azipunguze. Allah alikubali kupunguza sala hizo, mara ya kwanza Allah alipunguza sala tano, Mtume anaporejea kwake mara ya pili Allah alipunguza sala hadi zikasalia tano kwa siku. Mtume kupokezwa sala ni tukio la kuogofya mno. Ni suala la ajabu, ambapo Allah mwenyewe alizipunguza sala hadi tano kwa siku. Mtume alionyesha ushujaa wa

kipekee kwa kuweza kuzungumza naye Allah. Kwanza alipopewa nafasi anasema haja ya moyo wake, hakupoteza muda. Aliwasilisha takwa lake kwa Allah. Kisha akamsihi Allah kuupunguzia umma wa Mtume sala kwa siku. Jamii ya Waislamu wanaamini kuwa hakuna mwanadamu, awezaye au aliyewahi kufanya matendo kama ya mtume Muhammad ndio sababu ni matukio ya kipekee.

## 4.3 Mandhari ambayo yanaaogofya na kushangaza

Mandari ya mbinguni yanaogofya na kushangaza, japo kuna machache yaliyotajwa katika mbingu ya kwanza hadi ya sita, tunakisia kuwa huenda mbingu hizo zilimwogofya Mtume mno. Maajabu aliyoyaona Mtume, yamedokezwa katika mbingu ya saba, ambapo Mtume anasema hata malaika hangeweza kuendelea mbele ila yeye tu. Anapoendelea peke yake, anakuwa mwepesi hata kuliko mawazo, anapitia katika uwanja mkubwa uliogawika mara mbili; eneo moja la uwanja huo linawaka taa na lingine limejaa giza tupu. Anazidiwa na woga na ukimya kwa sababu ya kuwa pweke. Mara hii anajiwa na wimbi la furaha, yaliyofuatia ni manukato mazuri yaliyonuswa na Mtume pekee. Mazingira haya yanamtia Mtume hofu na woga kweli kweli.

## 4.4 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo,* mhusika Liyongo hajitokezi katika muktadha finyu wa jamii moja. Hali hii imejitokeza ili kuondoa ufinyu wa ujumbe ili usiwe wa watu au wa jamii moja tu bali uwe kwa manufaa kwa watu wengi. Watu wanafaidika kutokana na tamaduni na desturi mbalimbali, wala si tamaduni au mila finyu za jamii moja. Hadi hii leo, jamii nyingi zinampigania Fumo Liyongo na kudai kuwa ni wao. Kwa kila namna wanajamii hao walitaka kutambulika au kuhusishwa na ukoo wa shujaa huyu. Kwa hivyo, watu wengi wananufaika na sifa za shujaa huyu, bila kuwepo na mipaka ya ukoo fulani, mipaka ya mahali au jiji fulani. Liyongo ni mhusika wa jamii pana ya watu wanaotoka katika makabila mengi wenye mila, desturi na tamaduni tofauti tofauti. Katika utenzi huu Liyongo anajitokeza katika jamii ya Wadahalo na Wagalla, hivyo kuvunja mipaka ya mahali.

Kuna kuvunjwa mipaka ya kimahali katika utenzi huu kwa sababu matukio yaliyomo hayajajikita katika mahali mahususi. Kwa mfano mtunzi anazungumzia mandhari ya kisimani anapofia Liyongo, mazingira ya gerezani ambapo Sultani anamtia Liyongo,

akingojea kuuliwa. Liyongo anapogundua njama ya Sultani ya kupanga kumdhuru anahama Pate na kutorokea mwituni ambapo anaishi na Wasanye na Wadahalo. Liyongo anasafiri kutoka bara kuelekea Pate. Tena anarejea bara anapobaini njama ya Sultani ya kutaka kumdhuru. Ni wazi kuwa utenzi huu unarejelea matukio yanayotendeka katika mazingira mbalimabli na hivyo kuvunja mipaka ya kimahali. Wanajamii pia walitoka nyumbani mwao, ili kwenda kuchota maji kisimani hivyo wakawa wametoka mahali pamoja na kuelekea kwingine. Katika kudhihirisha kuvunjwa kwa kanuni hii, mtunzi anasema kuwa Liyongo alizaliwa Siu, kisha akaenda Pate kutembea na akakumbana na kifo chake kwa Mwana:

> ya Liyongo hukwambiya
> Siu alikozaliwa
> Pate akitembeleya
> Kwa Mwana akafiliya (ub.230).

Sifa nzuri za Liyongo pia zinafahamika mbali na karibu. Sifa hizi hazikubakia kule Liyongo alikozaliwa tu. Wagalla waliposikia sifa hizo wanatamani kumwona hata wanatamani mbegu yake. Wanataka awaolee msichana wao. Sultani naye anajawa na hofu ya kuondolewa mamlakani, kwa sababu ya sifa nzuri za Liyongo zilizoenea ambazo zilimpelekea kupendwa na watu wengi. Watu wa karibu na wa mbali, watu waliotokana na ukoo wake na wasiotokana nao walizienzi nyimbo za *Gungu* alizoziimba Liyongo. Mapenzi ya nyimbo hizo yalivunja mipaka ya mahali kwa kuimbwa na jamii nyingi. Inasemekana kuwa baadhi ya jamii za waswahili zingali zinaimba nyimbo hizo hadi hii leo.

### 4.5 Kuvunjwa kwa mipaka ya mahali katika *Ukawafi wa Miiraji*

Matukio katika *Ukawafi wa Miiraji* hayajajidhihirisha katika kijiji kimoja, nchi, jumuiya au bara moja bali ni matukio yenye upana wa dunia nzima. Hali hii imejitokeza ili kuondoa vikwazo vya kitamaduni, mila na desturi za jamii moja au mbili ambazo ni finyu. Kuna kuvunjwa kwa mipaka ya mahali. Hii ni kwa sababu safari ya Miiraji inaanzia duniani na kuelekea mbinguni. Kwa hivyo, matukio katika utenzi huu hayajajikita katika mandhari fulani mahususi. Ujumbe wa wito wa Mtume ulifanyika duniani, alitakaswa akiwa duniani na safari yenyewe inaanza kuelekea mbingu ya kwanza hadi mbingu ya saba na kurejea duniani.

Sifa za mtume Muhammad zilisambaa kote duniani na mbinguni. Kwa mujibu wa utenzi huu Muhammad ndiye Mtume wa pekee wa Allah, ambaye anatambulika. Yeye ndiye Mtume wa kwanza na wa mwisho zaidi yake hakuna Mtume mwingine. Sifa hizi za Mtume zinajulikana mbinguni na kwa mataifa ya Kiislamu duniani na hivyo kuvunja mipaka ya mahali. Mtume alijiwa na malaika akiwa duniani Makkah, usiku alipokuwa amelala, alijiwa mara tatu, kisha anatakaswa. Anapotakasika anapanda buraki na kuelekea mbingu ya kwanza. Mara kwa mara, aliwaongoza malaika katika sala. Alipofika katika mbingu ya kwanza alipokewa naye Adam ambaye alimkaribisha kwa heshima na upendo. Safari ikaendelea hadi mbingu ya pili ambapo alikutana nao Isa na Yahya ambao waliinuka kumpokea Mtume. Kisha akendelea hadi mbingu ya tatu, ambapo walipokewa na Yusufu. Kisha akaendelea hadi mbingu ya nne ambapo alilakiwa naye Idirisi. Wakaenda mbingu ya tano ambapo walipokewa na Haruni ambaye aliwakaribisha kwa taadhima kubwa. Wakasali kisha wakaelekea mbingu ya sita. Walipofika walipokelewa na Musa. Mtume alionyeshwa jeshi la Musa ambalo hakuona mwisho wake. Kisha akarithishwa jeshi hilo kubwa kuwa lake. Hatimaye wakafika mbingu ya saba. Huko walipokewa na Ibrahimu ambaye alimtaja Mtume kama nduguye. Mtume akaendelea hadi kipeo cha safari yake ambapo alipewa sala alizoomba zipunguzwe hadi tano na Allah. Baada ya kupewa sala hizo alirejea ili kuiletea jamii yake na dunia nzima. Matukio ambayo tumeyajadili yanaonyesha kuvunjwa kwa mpaka wa mahali.

Safari ya Mtume inaanza duniani kuelekea mbinguni, anapewa sala naye Allah na kisha kurejea duniani. Hakuna mpaka katika safari hiyo ya duniani na mbinguni. Aidha jeshi la Musa ambalo Allah anampatia Mtume halina mwisho wake. Mtume anajaribu kutaka kuona mwisho wake, lakini anakosa mpaka wa mahali ambapo jeshi lenyewe limeishia. Sala anazopokezwa Mtume, zinavunja mipaka ya mahali kwa sababu anazileta duniani kwa ajili ya watu wa jamii yake. Watu hao wanaweza kuwa Waislamu wa ulimwengu wote. Sala ambazo zinafaa watu wote duniani bila kuzingatia mipaka ya mahali. Kutokana na mifano tuliyoitoa, kwa maoni yetu tunaonelea kuwa mpaka wa mahali umevunjwa na haupo.

### 4.6 Matukio ya kifantasia katika *Utenzi wa Miiraji.*

Katika utenzi huu, kuna matukio ambayo yanawezekana katika ulimwengu wa kimawazo. Huenda mwandishi alipandwa na mihemko ya kimawazo. Mtume

kupasuliwa kifua na kushonwa wakati huo huo, awe amepona kabisa alama yeyote isionekane ni tukio linalowezekana katika fikra tu. Hii ni kwa sababu namna mwandishi alivyoeleza matukio hayo haiwezekani kutendeka katika hali halisi kwa mtu yeyote duniani.

Mtume alipanda buraki ambaye alimsafirisha hadi mbinguni. Akiwa safarini aliona matukio mbalimbali ambayo ni ya kimawazoni tu. Mtume alionyeshwa Jahanam ambapo aliona moto uwezao kuteketeza hata mawe. Ndaniye aliwaona watu ambao ni waovu. Pia Mtume alionyeshwa watu ambao walikatwa ndimi zao na wakati huo huo zikamea tena. Aliwaona watu walioparura nyuso zao na kujiumiza vibaya. (ub.28-33), Malaika alimweleza kuwa hao ni waovu siku ya kiama watabaki na mifupa mitupu nyusoni mwao. Waliendelea na safari hadi mbingu ya kwanza. Alipokewa na Adamu. Kisha waliendelea hadi mbingu ya saba, ambapo Ibrahimu aliwalaki. Tena Mtume alipata nafasi ya pekee ya kuzungumza na Allah, ambaye alimpa sala. Mtume alimrai Mungu ambaye alikubali kuzipunguza. Matukio ambayo tumetaja na mengine mengi katika utenzi huu ni ya mawazoni. Hivyo, yanawezekana katika hali ya kifantasia na haiwezekani matukio kama hayo kutendeka katika ulimwengu halisi. Tunatarajia kuwa matukio haya na mengine katika utenzi yameweka wazi sifa za uhalisiajabu ambapo mengi ya matukio hutendeka kutokana na mtunzi kupandwa na mihemko ya kinjozi.

### 4.7 Matukio ya kifantasia katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.*

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, matukio mengi yanayozungumziwa ni ya kifantasia, kwa sababu sifa za unene, sifa za kubashiri mambo alizo nazo Liyongo, sifa za uwezo au nguvu za kimwili ni za kufikirika tu. Mtunzi anasema kuwa Liyongo alikuwa na uwezo wa kubeba vitu ambavyo vingejaa nyumba nzima (ubeti wa 37). Vile vile alitembea kwa haraka mno; usiku au mchana kutembea ni sawa na angetembea kutoka Shaka hadi Pate kwa siku mbili tu. Sifa ya Liyongo ya kutodhurika kwa silaha yoyote ni tukio lisiloaminika katika hali halisia. Lawezekana tu katika mawazo. Liyongo angewapiga maadui wake, huku wao wakimchoma mkuki na silaha nyinginezo asidhurike. Walijaribu kumuua lakini ikawa kazi bure. Madai kuwa ni sindano ya shaba ndio iwezayo kumdhuru Liyongo ni ya kifantansia. Aidha Liyongo kuyajua mawazo ayawaziayo mtu na matukio ya baadaye ni sifa aliyo nayo ambayo ni ya kifantasia. Kwa mujibu wa *Utenzi wa Fumo Liyongo* aliweza kubaini

yatakayomfika mwanawe baadaye, alikuwa ameshajua mipango ya mwanaye ya kumsaliti. Aidha Liyongo alijua mapema kuwa Sultani alipanga kumdhuru ndio akatoroka Pate:

> Liyongo akatambuwa,
> Huzengea kuuawa,
> Pale pate kayepuwa,
> Barani akitembea (ubeti wa50)

Pia anagundua njama ya Wadahalo na Wasanye ya kutaka kumuua kwa kumfuma mshale. Sifa hii ya Liyongo kujua wanayowazia watu kumhusu ni ya kufikirika tu.

### 4.8 Wakati hausongi katika kazi ya uhalisiajabu

Matukio katika *Utenzi* wa *Fumo Liyongo* huonyesha kuwa wakati hausongi kwani muda matukio yalichukua katika utenzi haueleweki. Mtunzi hajafafanua kuwa ni muda kiasi gani Liyongo alitiwa gerezani. Hatujui Liyongo alikaa mwituni miaka au siku ngapi. Aidha vipindi alivyoishi katika maisha yake havijabainishwa katika utenzi. Kwa hakika kipindi cha wakati kilichotajwa katika utenzi ni siku mbili tu ambazo Liyongo alisafiri kutoka Shaka hadi Pate. Lakini matukio yote kwenye utenzi hayajulikani ikiwa yalichukua miaka, siku, majuma, miezi au saa. Hata Liyongo anapoaga dunia mtunzi anadokeza kwamba watu wanaomboleza lakini hataji ni kwa kipindi cha muda gani.

Katika utenzi wa *Ukawafi* wa *Miiraji*, mbali na mtunzi kueleza kuwa safari ya Mtume ilichukua usiku mmoja tu, yapo matukio mengine ambayo muda yalichukua haueleweki. Kama vile, mtunzi hakufafanua ni saa ngapi Mtume alitumia akiwa katika mbingu ya kwanza, ya pili , ya tatu hadi ya saba. Yeye anadokeza kuwa Mtume alisafiri hadi mbingu ya saba. Aidha hatujui ni muda wa kiasi gani alichukuwa alipokuwa anapewa sala, akarudi kwa Allah, anashuka hadi mbingu ya sita alipo Musa, tena akarejea kwa Allah mpaka zikapunguzwa kuwa sala tano kwa siku. Matukio mengi katika utenzi huu ni kama muda hausongi kwani hatuelekei kufahamishwa ni tukio lipi lilichukua muda gani.

## 4.9 Upanuaji wa mwanda wa kisimulizi

Wamitila (2008) anatoa rai kuwa, huwezi kuhusisha matendo ya fasihi ya ulimwengu wa kifantasia au ulimwengu wa kufikirika na matukio ya ulimwengu dhanifu yaingiliane na matukio ya ulimwengu halisi.

Katika *Ukawafi* wa *Miiraji,* Sifa hii ya upanuaji wa mawanda ya kisimulizi inakiukwa kiasi kwamba mtunzi anazungumzia matukio ya mbinguni na ya duniani bila kuweka mpaka kati yao. Matukio ya duniani yanaingiliana sana na matukio ya mbinguni. Isitoshe si matukio ya mbingu moja tu bali ni mbingu ya kwanza, ya pili hadi ya saba. Mbingu saba na dunia zinaingiliana kiasi cha kufikirika kuwa ni miji au mitaa miwili jirani. Kujiwa kwa Mtume usiku, kupewa ujumbe, kutakaswa na kuanza safari kutoka Makkah hadi Jerusalem na kisha kukwea mbingu ya saba inachukua muda mfupi mno. Kwa hakika hizi ni sehemu mbili zilizotengana kwa mbali sana. Lakini katika utenzi huu, kipindi cha usiku mmoja anaouchukua Mtume kinavunja mpaka wa mawanda wa kisimulizi.

Aidha, mtume Muhammad anadhihirisha kuvunjwa kwa mpaka huu alipofika katika mbingu ya sita, ambapo Musa alimshauri arejee kwa Allah kwa sababu kutakuwa na watu wa jamii yake hawangeweza kumudu sala hamsini kwa siku. Alipomwomba Mola wake kuzipunguza sala hizo, alikubali kuondoa sala tano. Mtume alirejea alipokuwa malaika Jibrili ambaye anamwongoza tena hadi mbingu ya sita kukutana na Musa. Wakati huu Musa alimshauri Mtume kwenda kwa Allah mara ya pili ili sala hizo zipunguzwe zaidi. Bila kupoteza wasaa anarudi huko huko katika mbingu ya saba ambapo Allah alikubali kupunguza sala hizo hadi tano. Mtume alisafiri mara kadha kwenda mbingu ya saba na kurudi kisha kurejea huko kwa muda mchahe mno. Mbingu hizi mbili zilisimuliwa kwa namna inayoashiria kuwa ziko karibu sana kama miji jirani. Safari ya Mtume kwenda mbingu ya saba na kurejea tena na tena, ni dhihirisho tosha la kuonyesha kuvunjwa kwa mpaka wa mawanda ya kisimulizi. Sehemu hizi mbili zinahusisha matukio yaliyotendeka kwote kana kwamba ziko pahali pamoja.

**Hitimisho**

Katika sura hii, tumeonyesha sifa za kiuhalisiajabu jinsi zinavyojitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Sifa hizo ni kama vile, matukio yanayoogofya na kushangaza, kuvunjwa kwa mipaka ya mahali, matukio ya kifantasia, wakati wa kiduara na upanuaji wa mawanda ya kisimulizi. Sifa hizi zilidhihirika kwa mhusika Fumo Liyongo pekee katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ilihali katika *Ukawafi wa Miiraji* kwa takribani wahusika wote.

## SURA YA TANO

## UMUHIMU WA SIFA ZA KIUHALISIAJABU KATIKA *UKAWAFI WA MIIRAJI* NA *UTENZI WA FUMO LIYONGO*

### 5.0 Utangulizi.

Baada ya kuangazia sifa za uhalisiajabu katika,*Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji* tumedhamiria kutathimini umuhimu wake miongoni mwa wanajamii. Sifa hizi za uhalisiajabu huadilisha wanajamii. Wanajamii huwa na matumaini ya kuishi na kufurahia maisha mema ya baadaye kuliko ya sasa. Watu huburudika, hupendana na kujitambulisha kwa kuhusishwa na sifa hizi. Sifa hizi hutawala mifumo ya kijamii kama vile dini, elimu, siasa, mila, tamaduni, na mifumo mingine. Tumesukumwa kuamini kuwa sifa hizo zinaweza kuwa na umuhimu mkubwa kwa wanajamii ambazo tutazifafanua hapa chini.

### 5.1 Fahari kwa wanajamii na waumini wa dini.

Uhalisiajabu ni fahari kubwa kwa waumini wa dini husika, kwa kuwepo kwa sifa hii, waumini hujawa na majivuno ya imani zao katika dini wanayoshiriki. Kwa mfano, katika *Ukawafi wa Miiraji,* waumini wa dini ya Kiislamu, wanafaharikia sifa zinazomwandama mtume Muhammad. Sifa anazopewa Mtume, zinawafurahisha wafuasi wake ambao ni Waislamu. Mtume anapewa nafasi ya kipekee ya kupanda mbingu zote saba. Mtume ndiye aliyepata nafasi ya kipekee ya kuzungumza na Allah. Aidha kwa mujibu wa utenzi wenyewe yeye, ndiye Mtume wa kwanza na wa mwisho mbele yake au nyuma yake hapana mwingine. Hali hii ya upekee wa Mtume Muhammad unawafanya wafuasi wake kuwa na furaha tele katika imani ya dini yao. Abdullah (2010) anasema, Kuran na usemi wa Mtume ni hekima isiyo kikomo kwa jamii itakayodumu milele. Tunakubaliana na maoni ya mtaalamu huyu, japo madai yake lazima yahusishwe na mwislamu mwaminifu, madai yanayoungwa mkono na ukawafi wenyewe (dibaji katika *Ukawafi wa Miiraji*). Dini ya kiislamu imeshamiri kwa watu wote na kabila zote duniani. Kusambaa huku kunatokana na watu wengi kuionea fahari na kutaka kujihusisha na sifa za mtume Muhammad.

Mtume kujiwa na malaika, kuamshwa mara tatu, kupasuliwa kifua, kutakaswa kisha kushonwa ni tukio la uhalisiajabu ambalo linawafanya wafuasi wa dini ya kiislamu kuwa na fahari. Tukio hili linawafanya waumini hawa wawe na majivuno kwa sababu wanaamini kuwa hakuna mtu mwingine yeyote ambaye amewahi kujiwa na malaika

kama alivyojiwa Mtume. Swala hili la kutofananishwa na mwingine ni la kujivunia mno hasa kwa wafuasi wake (sura 17:1). Mtume Muhammad kubebwa na buraki ni jambo la kujivunia. Kwa mujibu wa utenzi, hapajawahi kuwepo na mnyama kama buraki, mwenye sifa za kipekee. Kwa misingi hiyo tunakisia kuwa, pengine Allah alimuumba mnyama huyu kwa ajili ya Mtume pekee katika usiku huo wa Miiraji.

Mtume kuteuliwa naye Allah kwenda hadi upeo wa juu kabisa katika safari ya mbingu saba ni tukio la kujivunia. Mtume Muhammad anachaguliwa miongoni mwa umati wa watu duniani kote. Isitoshe anapaa hadi mbingu ya saba, hata zaidi ya malaika mkuu Jibrili ambaye hakuruhusiwa kuufikia upeo Mtume alifika. Kwa mujibu wa *Ukawafi wa Miiraji* Mtume alipata nafasi ya kuonana na Allah uso kwa uso alipokuwa anapewa sala. Kwa tukio hili, wafuasi wa dini hii hawana budi kujivunia. Aidha mazungumzo yalifanyika huku Mtume akienda mbingu ya sita na kurudi kuzungumza na Mola wake hadi alipompunguzia sala. Ni tukio la kujivunia kwa sababu wafuasi wa dini ya Kiislamu wanasali idadi ya sala hizo kwa uaminifu hadi hii leo. Muhammad ana ushujaa wa kujadiliana na Allah kuhusu idadi ya sala angepelekea umma wake. Majadiliano ya Mtume na Allah hayakufanyika mara moja tu bali mara kadhaa. Hili linamsawiri kama shujaa wa dini ya Kiislamu, kwa hivyo wafuasi wake wana kila sababu ya kujivunia shujaa wao.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* sifa za uhalisiajabu zinasababisha jamii iliyomzaa na kumlea Liyongo kutambulika. Aidha sifa hizi za kiajabu zinawakilisha jamii yake katika ngazi ya kitaifa na kimataifa. Kulingana na maoni yetu, haiwezekani kupambanua sifa za kiajabu za Fumo Liyongo, pasi na kutaja mfumo mzima wa jamii ya Waswahili. Kwani sifa hizo ni kama viwakilishi vya jamii hiyo. Jamii ya Waswahili inatambulika kote duniani kutokana na kutaja sifa za ajabu za Fumo Liyongo. Ni maoni yetu kuwa sifa za Fumo Liyongo ni muhimu kwa jamii ya Waswahili ambapo iwapo zitaondolewa jamii husika itabakia na pengo lisilozibika milele. Pengine mtu au watu huenda wakakosa kufahamu sifa za Waswahili pasipo kutaja sifa za Fumo Liyongo. Baadhi ya mila za jamii ya Waswahili zimejikita katika sifa za shujaa huyu. Hata kama Liyongo aliishi miaka mingi iliyopita, sifa zake za kiajabu ndizo zilizosababisha jamii ya kimataifa kuvutiwa na jamii ya Waswahili. Kwa mfano Edward Steere (1970), miongoni mwa wazungu wengine walikusanya taarifa kuhusu Liyongo na kuzihifadhi katika maandishi.

Kwa upande wake Steere (187: VI) anatoa rai kuwa Waswahili wanajitambulisha pakubwa na Liyongo. Kujitambulisha huku kunatokana na sifa za kushangaza alizokuwa nazo Liyongo, kwani pasipo sifa basi mtu hatambuliki tena. Sifa zake za kiajabu bado zingalipo, miaka mingi baada ya kifo chake. Sifa zake zingali zinaathiri hisia za nafsi za watu katika jamii ya Waswahili. Wasegeju, Wapokomo, na Wabajuni wote kila mojawapo wa jamii hizi wamo mbioni kutaka kujitambulisha na Liyongo kwa sababu ya sifa za kushangaza zilizomwandama. Hata hivyo Liyongo alionekana kuegemea katika jamii ya Waswahili ambayo ilimwajabia mno mbali na kumwonea fahari.

## 5.2 Kitambulisho cha kidini na kijamii.

Katika *Ukawafi wa Miiraji* sifa za kiuhalisiajabu ni kitambulisho cha kidini hasa dini ya Kiislamu. Ni mtazamo wetu kuwa, kila imani duniani ina sifa zinazoitambulisha. Tumegundua kuwa dini ya Kiislamu ina sifa ambazo zinajitokeza katika *Ukawafi wa Miiraji* na ambazo zinaipatia dini kitambulisho. Aidha safari ya Miiraji ni mojawapo ya sherehe ambazo zinasherehekewa na waumini wa kiislamu hadi hii leo. Waumini hukusanyika hasa nyakati za usiku huku wakikaririana safari ya Miiraji. Nchi zingine duniani kama vile Indonesia huhesabu siku kwa kuzingatia kalenda ya Kiislamu na kuuweka usiku wa Miiraji kuwa siku kuu (siku ya ishirini na saba ya mwezi wa Rajab) Kwa kufanya hivyo jamii/nchi, hujitambulisha na imani ya kiislamu. Mtume Muhammad anajiwa na Malaika ambao wanamtakasa, kisha kumuamrisha apande buraki kwenda mbinguni ambaye ni mhusika katika utenzi. Inasadifu kuwa yeye ndiye kiongozi Mtume wa kipekee aliyetambulika kwa waumini wa dini ya kiislamu. Aidha miji aliyohusishwa nayo Mtume Muhammad kama vile Makkah ni kitovu kikuu cha dini ya kiislamu. Kuna mshikamano wa moja kwa moja wa idadi ya sala alizopokea mtume Muhammad na zile ambazo zinashirikishwa na waumini wa dini ya kiislamu. Ni wazi kuwa kila muumini wa dini hii anajitambulisha na mtume Muhammad.

Allah, malaika Jibril, mitume kama Isa, Idris, Haruni, Musa na wengine ni wahusika wa kiajabu ambao wametajwa katika Kuran Tukufu kama mitume wakuu; kutajwa huko kunahusu mchango wao katika kuisambaza dini ya Kiislamu (Sura 19:28). Mungu anawaamrisha Malaika Jibrili na wengine kumjia mtume Muhammad. Mjo huu ulikuwa ndio mwanzo wa safari muhimu katika kuteuliwa kwa mtume

Muhammad. Safari hii iliandaliwa kwa ajili ya Mtume kwenda kuchukua sala. Sala ambazo ni kigezo muhimu katika dini. Aidha Mtume alionyeshwa mazingira ya ahera jinsi yalivyostaajabisha. Kuna watu anuwai ambao walipewa adhabu mbalimbali kulingana na matendo yao duniani. Haya ni matukio yanayofungamana na dini ya kiislamu kwani waumini wa dini ya kiislamu wanaamini kuwa mtume Muhammad ndiye Mtume wao. Aidha wao husali mara tano kwa siku. Ni maoni yetu kuwa waumini wa Kiislamu wanakubaliana na matukio haya ya kiajabu kuwa ya kweli na wanajenga imani yao kwayo.

### 5.3 Ukombozi, uzalendo na undugu baina ya wanajamii.

Katika *Ukawafi wa miiraji*, kuna matukio ya kushangaza ambayo yanamzingira mtume Muhammad. Tukio la Mtume kupanda mbinguni linavutia watu wa makabila na mataifa mbalimbali duniani.Watu hawa wametokana na tamaduni tofauti tofauti ambao hatimaye hujumuika katika imani moja kwa misingi ya kidini. Aidha wafuasi hawa hawatoki katika taifa wala bara moja bali wanatokana na mabara na mataifa tofauti tofauti. Safari ya Miiraji imewavutia watu wa mila na desturi tofauti tofauti katika dunia nzima.

Katika Kuran Tukufu, Allah anauita undugu wa Waislamu (Mu'minoon), lenye maana kuwa wale wanaomwamini Allah na Mtume wake wamejumuika kwa undugu wa kiislamu. (Kuran sura 49:10) Aidha anaongezea kwa kusema kuwa wafuasi wa kiislamu anawataja kuwa (awliyyaa') lenye maana wafuasi wenye undugu: wanaoungana wao kwa wao, katika muungano wenye msingi wa uislamu. Waumini wawe wa kike au wa kiume, wote wanatunzana wao kwa wao, wanasali pamoja, wanatoa Zaka na kumtii Allah na Mtume wake. "Binadamu wote kuanzia Adam hadi Hawa, Mwarabu hana uspesheli juu ya asiye Mwarabu, pia mweupe si muhimu kuliko mweusi. Jifunze kuwa kila mwislamu ni ndugu kwa mwislamu mwenzake (Kuran 9:72). Kwa hivyo wanamfwata Mtume na kutii mafunzo yake kama mteule wa Allah. Watu wa mataifa tofauti huishia kuunganika chini ya imani moja ya Kiislamu, kuunganika katika imani hii, waumini hao huwa na undugu baina yao. Katika kufanya hivyo watu huwa wameungana chini ya mtume Muhammad. Watu hawa wanachukuliwa kama wale waliofaidika kutokana na Mtume kuomba kupunguzwa kwa sala nyingi ambazo zingekuwa mzigo mzito kwao. Kupunguzwa kwa sala hizo

kwa waumini wa Kiislamu kuliashiria kukombolewa na mzigo ambao hawangeweza kutekeleza kila siku. Waumini walipewa sala tano ambazo ni kazi rahisi isiyowachosha.

Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo*, uhalisiajabu unaleta muungano, uelewano na undugu baina ya wanajamii. Jamii ya Fumo Liyongo ilikuwa imegawanyika kabla ya kuzaliwa kwake. Kilichowaunganisha zaidi ni nyimbo zake ambazo walizipenda mno. Umati wa watu ulikusanyika mara tu waliposikia kuwa Liyongo anaziimba. Kwa mfano alipokuwa ametiwa gerezani watu wengi wanatokea ili kusikiliza nyimbo zake za gungu:

Wute wakakutanika,
mahala pakatandikwa,
na uzuri wakaweka,
deuli na subahiya.( ubeti wa 113)

Wakatandika za zari,
na libasi za Hariri,
wakaimba mashairi,
ngoma na kusi pamoya (ubeti wa 114).

## 5.4 Kuimarishwa kwa dini ya kiislamu.

Matukio ya kushangaza katika *Ukawafi wa Miiraji* yamejengwa ili kuimarisha imani ya waumini wa Kiislamu. Mtume anaonyeshwa adhabu mbalimbali ambazo watu wanapewa ili kulipia matendo yao maovu. Kwa mfano alionyeshwa kundi la watu ambao ndimi zao zilikuwa zikikatwa kutokana na matendo yao maovu. Tukio hili na mengine ni kama onyo kali kwa watu wasitende maovu ya aina hiyo. Kwa hivyo imani ya dini yao inaimarika.Waislamu wana imani kuwa wanadamu wote wanaotenda kinyume na matakwa ya Allah wataadhibiwa vikali:

Kisha wakenenda wakaona watu dhamima,
Wakipondaponda vitwa vyao nyundo za chuma,
Jiburilu kamba: ni wazito wa sala kwima,
Hawatoi zaka, mali yao Jehannama (ubeti wa 19).

Mtume anaongoza sala kila wakati alipoambiwa na malaika kufanya hivyo. Dua hii ya Mtume, pia huwa ni njia mojawapo ya kuimarisha imani ya Kiislamu. Aidha kwa mujibu wa Kuran dua ni kigezo muhimu sana katika kuimarisha imani ya waumini:

Watumishi wangu wakiuliza maswali kunihusu, basi nitawasikiliza na kuwapa hitaji la moyo wao (Kuran 2:186)

Allah anawatuma malaika ambao wanamjia Mtume, kwa uwezo alio nao Allah, malaika anapewa uwezo wa kumpasua, kumtakasa na kumshona Mtume.Utakaso huu ndio maandalizi ya safari ya Mtume kupanda hadi mbingu ya saba. Kupanda huku kunafanyika kwa haraka mno, hii ni kutokana na uwezo mkubwa alio nao Allah. Matukio haya ya ajabu yanaimarisha imani ya waumini wa kiislamu. Anayekumbana na tukio hili anakuwa na taswira ya Mungu kama mwenye nguvu anayewainua waliodunishwa hadi upeo wa juu kabisa hata kushinda malaika. Mtume alikuwa kiumbe mwenye sifa na hisia za kibinadamu, anatakaswa hadi anatakasika kushinda malaika. Kwa hili muumini anakuwa na hamu ya kutakazwa na kuinuliwa hadi upeo wa mbingu ya juu alivyoinuliwa Mtume. Mtume anapojaribiwa kwa chakula, yeye hababaiki, alifanya uchaguzi mwafaka. Akachagua maziwa badala ya divai. Tendo hili linawamotisha wafuasi wa dini ya kiislamu kuwa wanafaa kufanya uchaguzi mwema mara tu wanapojaribiwa. Kwa Allah kuridhia ombi la Mtume na kupunguza sala ni tukio la kiuhalisiajabu ambalo linakuza imani ya muumini wa dini ya kiislamu. Muumini wa kweli atakuwa na tumaini la ombi lake kujibiwa naye Allah ikiwa atatii matakwa yake.

### 5.5 Kielelezo mfano cha kuigwa.

Inaaminika kuwa Korani tukufu imeandikwa kutokana na maono aliyofunuliwa mtume Muhammad. Chittick na Murat (1994:81-82) wanasema "Kuwa mwanadamu kamili ni kutekeleza matendo ya uungu alivyotenda Mtume." Ni wazi kuwa maandishi yaliyomo, kwenye Kuran yanatoa mwongozo wa maisha jinsi mwislamu alivyostahili kuishi. Aidha inamtaja Mtume kama kielelezo bora cha kuigwa. Katika *Ukawafi wa Miiraji*, uhalisiajabu umechangia pakubwa katika kukuza kielelezo mwafaka cha kidini ambacho waumini wa dini ya kiislamu wanastahili kuiga. Kwa mujibu wa utenzi wenyewe, mtume Muhammad, alikubali kuwapokea malaika ambao walipasua kifua chake kisha wakamtakasa. Hatimaye aliitikia ujumbe wao. Bila kusita alijiandaa kwa haraka na kuanza safari usiku huo huo. Kutokana na utakaso Mtume alipokelewa na mitume wengine katika kila mbingu hadi mbingu zote saba. Mbali na mapokezi haya, Mtume alionyeshwa jahanamu na watenda maovu wakilipia matendo yao. Hatimaye alipewa sala anazopelekea jamii yake. Kwa hili,

Mtume alidhihirika kuwa mchaguliwa ambaye alikubalika kwa matendo yake. Yeye ndiye Mtume wa kwanza, zaidi yake hapana mwingine. Alipojaribiwa, Mtume alifanya uchaguzi mwema. Muda wake mwingi aliuchukua katika maombi na kutii wito wa mola wake. mtume Muhammad alitoa mwelekeo mwema wa kuigwa na wafuasi wa dini hii hasa kwa watu wote walio na hamu ya dini ya Kiislamu.

### 5.6 Historia ya jamii husika.

Kutokana na sifa za kiuhalisiajabu, tunatoa rai kuwa jamii husika hupata nafasi ya kuielewa historia yao. Ni kweli kuwa fasihi ni kioo cha jamii, tenzi zikiwa mojawapo ya fasihi, ni mtazamo wetu kuwa jamii ya Waswahili hasa Waislamu hunafasika katika kuielewa historia ya jamii zao kutokana na tenzi hizi. Kutokana na sifa za uhalisiajabu katika tenzi, wanajamii hupata kufahamu mafanikio, dhuluma, mahangaiko na mengine ambayo wahusika lengwa walikumbana nayo. Changamoto hizi huwakumba wahusika mbalimbali katika tendi au kazi yoyote ya kifasihi. Sifa za wahusika hawa huchangia pakubwa katika kuipatia jamii hali au historia yake jinsi ilivyo. Kwa mfano sifa za kiuhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*, zilitupelekea kuangazia miji ambayo wahusika katika tenzi hizi walizaliwa, walikulia, walilelewa, walitembelea au kupigania. Kwa mfano katika *Ukawafi wa Miiraji* mtume Muhammad alitembelea miji kama vile Makkah, Badar, Yathribu, Medina na mingine. Kwa waislamu kuielewa miji hii, huwa ni njia moja ya kuelewa historia ya dini ya kiislamu halikadhalika ya jamii yao. Katika kutaja miji hii, jamii ya Waislamu hupata nafasi ya kufahamu chimbuko la dini hasa ni wapi ilipoanzia ambacho ni kiungo muhimu cha historia ya jamii yao.

Katika kupambanua sifa za kiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji*, majina ya watu na koo zao za karibu na mtume Muhammadi huchipuka. Majina ya watu kama Khadija, Abu Talib, Ayisha, Hafsa, Zeinab, Safiya, Abu Suffiyan, Al Abbas ni majina muhimu katika kuielewa historia ya Waislamu. Majina ya mitume wengine kama vile Haruni, Isa, Idris, Ibrahimu na Yahya pia huchangia pakubwa katika kuimarisha historia ya jamii ya Waislamu. Jamii ya waislamu hujielewa hata zaidi kwa kuuelewa ukoo uliosambaza dini yao na hivyo kufahamu historia yao.

Katika kuangazia sifa za ajabu zinazomwandama Fumo Liyongo, tunapata kujua miji ambayo Liyongo aliitembelea. Katika utenzi kumetajwa miji kama vile Pate,

Shaka, Ozi, miongoni mwa miji mingine. Aidha, tumeelewa kuwa kulikuwa na milima na kisima ambapo wanajamii walienda kuchota maji. Mbali na hayo, tunatajiwa majina ya vifaa mbalimbali kama vyungu, mafiga, mimea, miti na misitu katika mazingira alimokulia Fumo Liyongo. Vilevile, hali za maisha za majirani wake kama Wagala na Wadahalo pia zimeangaziwa. *Utenzi wa Fumo Liyongo* ulidokeza kwamba waliishi mwituni wakila matunda mbalimbali kama makoma. Mbali na sifa za kiuhalisiajabu jamii yake hupata nafasi nzuri ya kuielewa historia yao. Ngoma ya *gungu* alioicheza Liyongo ni kiungo muhimu katika historia ya Waswahili ambao wamekuwa wakiicheza hasa katika sherehe za harusi. Ngoma hii ya gungu ilichezwa saa za asubuhi wakati wa kuamkia siku ya kila mwaka.

**Hitimisho**

Sura hii imehusu umuhimu wa sifa za kiuhalisiajabu kwa wanajamii. Baadhi ya umuhimu tulioangazia ni kama vile, uhalisiajabu husababisha wanajamii kuionea fahari dini au jamii yao. Kupitia sifa za kiuhalisaijabu, wanajamii hujitambulisha na dini au jamii yao. Wanajamii hujikomboa, hupendana na huipenda nchi,dini au jamii yao kutokana na kuhusishwa na wahusika wenye sifa na kiuhalisiajabu. Imani ya wanajamii huimarika kutokana na kujihusiaha na wahusika wenye sifa za kiuhalisiajabu zinazowiana na imani yao. Aidha watu hupata vielelezo vya kuiga kutokana na kuwaiga wahusika wenye sifa za kiuhalisiajabu. Tulihitimisha katika sura ya sita na kuandika marejeleo baadaye.

## SURA YA SITA

### 6.0 Mahitimisho

Katika sura hii, tumetoa mahitimisho ya utafiti wetu ambao ulishughulikia sifa za kiuhalisiajabu na umuhimu wake katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji.* Tulifanya utafiti huu tukiongozwa na nadharia ya uhalisiajabu. Nadharia hii ilitufaa katika kuonyesha kuwa uhalisiajabu ni muhimu katika kujenga sifa za wahusika na mandhari katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa miiraji.*

Katika sura ya kwanza, tumeangazia mambo ya kimsingi yanayojenga utafiti wetu, tatizo la utafiti, sababu ya kuchagua mada, nadharia tete, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na njia za utafiti tulizotumia. Nadharia tete yetu ya utafiti huu ilikuwa sifa za kiuhalisiajabu katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji.* Ya pili ilikuwa, matukio ya kiuhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Ya mwisho ilikuwa, umuhimu wa uhalisiajabu katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utendi wa Fumo Liyongo* katika kuuendeleza ushujaa/dini.

Katika sura ya pili, ya tatu ya nne na ya tano, tumezitathimini kwa undani nadharia tete hizi katika kuchanganua mada yetu. Katika sura ya pili tuliangazia historia ya tendi, historia ya Waswahili, usuli wa mtume Muhammad alipozaliwa, alikolelewa, kuoa kwake, mapambano ya vita vya kidini na hatimaye Kisa cha Miraji kilichomo katika *Ukawafi wa Miiraji.* Pia tulihakiki kisa cha Fumo Liyongo jinsi kilivyo katika *Utenzi wa Fumo Liyongo.* Vile vile tulichanganua mazoea ya watunzi wa tenzi tukiegemea hasa *Utenzi wa Fumo Liyongo* na katika *Ukawafi wa Miiraji.* Tulitamatisha sura hii katika kuangazia dhamira ya mtunzi katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*, ambapo tulibaini kuwa katika *Ukawafi wa Miiraji* dhamira kuu iliopo ni kuimarishwa kwa dini ya Kiislamu ilihali katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni ushujaa wa kijamii.

Katika sura ya tatu, tulichanganua sifa za wahusika na mandhari katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* na *Ukawafi wa Miiraji.* Katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* tulibaini kuwa Fumo Liyongo ndiye mhusika pekee mwenye sifa za kiuhalisiajabu. Kwa misingi hiyo ilitubidi kuangazia sifa zake peke yake. Baadhi ya sifa zake ni: mnene ajabu, ana nguvu za sihiri, mpevu wa akili, hodari katika vita, alikuwa mtunzi na

mwimbaji wa tenzi. Aidha tuliangazia umuhimu wake katika utenzi wenyewe. Katika *Ukawafi wa Miiraji* tulichanganua sifa za wahusika wote, ambapo tuligundua kuwa utenzi huu una wahusika binadamu, wahusika wanyama na wasiokuwa na sifa za kibinadamu. Katika kundi la wahusika binadamu, tuliwaangazia mitume ambao walipatikana katika kila mbingu. Kwa mfano katika mbingu ya kwanza, palikuwepo na Adamu, ya pili wakapokelewa na Yahya na Isa, mbingu ya tatu wakamwona Yusufu. Wakaendelea hadi mbingu ya tano ambapo walilakiwa na Idirisi, wakafika ya sita huko wakapokewa na Musa na hatimaye wakaingia mbingu ya saba ambapo walilakiwa na Ibrahimu. Katika kundi la wahusika binadamu, tulichanganua sifa za mke mwema, mtume Muhammad, watu waovu na mitume wa mbinguni. Katika kundi la wahusika miungu, tuliangazia sifa za Allah na malaika. Katika wahusika wanyama, tuliangazia sifa za buraki. Hatimaye, tuliangazia umuhimu wa kila kundi au aina ya wahusika.

Katika sura ya nne, tulishughulikia sifa za kiuhalisiajabu. Tulifanya hivyo kwa kubainisha matukio ya ajabu ambayo yanatisha na kushtusha. Baadhi ya matukio yanayoogofya na kushangaza katika *Utenzi wa Fumo Liyongo* ni pale ambapo, mwandishi anasema kuwa mhusika Fumo Liyongo ni mnene kweli kweli, hadi Wagalla wanamfikia magotini. Liyongo aliweza kubeba vitu vingi ambavyo vingejaa nyumba na kutembea navyo kutoka Shaka hadi Pate kwa siku mbili tu. Inashangaza kuwa Liyongo anabeba vitu vingi kiasi ambacho haiwezekani mwanadamu wa kawaida kuvibeba na kutembea navyo kwa siku mbili hadi Pate. Liyongo anapuliza panda ya kwanza na ya pili hadi zinapasuka. Panda hizo zinatoa sauti ya kuogofya na kushangaza hadi umati wa watu unakimbia kuja kubaini hasa ni jambo gani limetokea. Ni jambo la kushangaza kwa Liyongo kupuliza panda hadi kupasuka. Aidha anawashangaza wengi kwa kuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kuwazuia askari zaidi ya mia moja katika vita na kuwashinda. Katika *Ukawafi wa Miiraji* kuna matukio ya kuogofya na kushangaza pia. Baadhi yao ni mjo wa malaika ambao walimjia mtume Muhammad wakipitia paani bila kuelewa jinsi walivyoingia chumbani. Aidha malaika hao, walimwamsha Mtume, wakapasua kifua chake, wakakitakasa kisha wakamtia mhuri wa utume. Utenzi unadokeza kuwa, wanamsafirisha Mtume kwa mnyama wa ajabu anayeitwa buraki. Wakiwa safarini Mtume anaonyeshwa matukio mbalimbali ya kuogofya na kushangaza. Mtume anaona watu waovu wakipiga vichwa vyao kwa nyundo,anaonyeshwa jahanamu,

anaendelea na safari ambapo anapokewa na mitume katika kila mbingu. Hatimaye anafikia upeo wa juu ambapo anakutana na Allah uso kwa uso. Ni jambo la kushtusha na kuogofya kwa Mtume kuonana na Mola wake ambaye anampa sala kwa ajili ya jamii yake.

Sifa nyingine ni kuvunjwa kwa mipaka ya mahali ambapo safari ya Mtume Muhammad inafanyika duniani na mbinguni. Mwandishi anasema kuwa Mtume aliamshwa alipokuwa amelala hadi mbingu ya saba ambapo alipokezwa sala na kurejeshwa ardhini. Tulionelea kuwa matukio yanayotajwa katika utenzi huu yanawezekana kuwa ya kifantasia kwa kuwa mtunzi hakuyashuhudia yeye mwenyewe, hivyo yawezekana pengine aliyawazia yaliyoandikwa katika *Ukawafi wa Miiraji.*

Sifa nyingine ya kiuhalisiajabu ni kuwa wakati hausongi kwa sababu haieleweka muda ambao mtume Muhammad alichukua katika mbingu ya kwanza, hadi ya saba na kurudi ardhini. Kuna wahusika ambao ni wa kiajabu kama vile Allah, mitume, malaika, buraki, watu waovu na mke mwema katika *Ukawafi wa Miiraji.*

Katika sura ya tano, tulibainisha umuhimu wa uhalisiajabu ambapo huwa na fahari kwa watu wa dini/wanajamii, hujenga historia ya jamii, huwa kitambulisho cha kidini/kijamii, huleta undugu, muungano na uzalendo. Uhalisiajabu huchangia pakubwa katika kujenga historia ya wanajamii. Tulionyesha kuwa uhalisiajabu huchangia katika kujenga kielelezo mfano cha kuigwa. Kwa ujumla utafiti huu umeangazia utafiti wa kiuhalisiajabu.

## 6.1 Mapendekezo

Katika *Ukawafi wa Miiraji* na *Utenzi wa Fumo Liyongo* tumezichanganua sifa za kiuhalisiajabu na muhimu wa uhalisiajabu. Tumeonyesha namna ambavyo mandhari na matukio ya kushangaza yanachangia katika sifa za kiuhalisiajabu. Hata hivyo tumeangazia umuhimu wa uhalisiajabu katika kuendeleza maudhui ya kishujaa/kidini. Tunapendekeza kuwa watafiti wengine waangazie umuhimu wa uhalisiajabu katika kuendeleza fani na maudhui katika tenzi hizi.

## 6.2 MAREJELEO


Abedi, A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: East African Literature Bureau.

Abdullah, S. A. (2010). *The sayings of Muhammad* . Whitefish, Montena: Kessinger publishing, LLC.

Abdulaziz, M.H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Allen, J.W.T. (1971). *Tendi: Six examples of a Swahili Classical verse form with Translations and Note.* London: Heinemann.

Breton, A. (1924). *Manifestoes of Surrealism. London:* University of Michigan Press.

Chittick, N. (1984). *Manda Excavations at an Island on the Kenyan Coast.* Nairobi: B.I.E.A.

Chittick, W.C., na Mulat, S. (1994) *Vision of Islam.* New York : Paragon House

Chiraghdin, S. (1977). *Marenga wa Mrima.* Nairobi: Oxford University Press.

Culler, J. (1975). *Structuralist Poetics.* London: Routledge and Kegan Paul.

Gibbe, A. G. (1990). "Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili", katika Gibbe, A. G. (Mh.) *Jarida la Kiswahili,* Juzuu 1. uk. 5.

Gatakaa, G. ( 2012). *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*: Nairobi. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Gichamba, J.M (2005). "Sifa za mashujaa na umuhimu wao kwa jamii zao: Ulinganishi wa Fumo Liyongo na Shaka Zulu." Chuo Kikuu Cha Nairobi. Haijachapishwa.

Harries, L. ( 1962). *Swahili Poetry.* London: Oxford University Press.

Hichens, W. (1972). *Al –Inkishafi S.A Nasir*. Nairobi: Oxford University Press.

Holman, C.H. (1960). *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey Press Inc.

Hussein, E. ( 1971). *Mashetani*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse.*London: Heinemman Ltd.

Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili Poetry" An investigation into the concept of East African Islam as reflected in the Utenzi* Literature. Leiden: E.J. Brill.

Miehe, G.N., n.k. (2004). *Liongo Songs: Poems Attributed To Fumo Liyongo*. Koln: Grudiger Koppe Verlag.

Magaju, J. (2004). *Uhalisiajabu katika ya Riwaya ya Babu Alipofufuka* (2001) ya S.A Muhammad na *Bina-Adamu! (*2002) ya K.W Wamitila. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mbatia, M. (2002). *Kamusi ya Fasihi.* Nairobi: Standard Textbooks.

Mberia, K. (2002). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publishers.

Mdee, J. S., n.k. (2009). *Kamusi Kamili ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mdee, J. S. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Mlacha, S.A.K. (1989). *Kiswahili katika Kanda ya Afrika Mashariki* : Dar es Salaam. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Mnyampala, E.M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Nairobi: Kenya Literature Bereau.

Muhammad, A. S. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili:Tamthilia, Riwaya na Hadithi fupi*: Nairobi: East African Educational Publishers.

Muhammad, A.S. (1995). *Amezidi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Muhammad, K. (1913). *Utenzi wa Fumo Liyongo. Dar es Salaam*: Tanzania Publishing House Ltd.

Mulokozi, M.M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es salaam: TUKI.

Mulokozi (1996). *Utangulizi wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M.M. & Kahigi, K. K (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing house.

Murray, P. (1978). *Literary Criticism*. Harlow Essex: Longman Group.

Mwangi. J. W. (2013) *Uhalisia na uhalisiajabu katika riwaya mpya*: *Babu alipofufuka* (2001) ya S.A. Muhammad na *Watu wa Gehenna* (2012) ya T.Olali. Tansnifu ya M.A Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Njogu, K. na Chimera, K. (1999). *Ufundishaji wa fasihi*: *Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K & Wafula, R.M. (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nurse, D. & Spear, T. (1985). "Reconstructing The History and Language of an African society." *The international Jounal of African History Studies*, volume 19. PP. 93-95.

Roh, F. (1925). *German Art in the 20$^{th}$Century*. Greenwich, Connecticut: New York Graphic Society Ltd.

Samweli, M. K. & Seleman, A. (2013). *Ushairi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es salaam university press.

Scott, A. F. (1983). *Current Literary Terms:* A Concise Dictionary, London: Macmillan.

Senkoro, F. E. M. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam. Dae es Salaam University Press

Sheikh, A. S. na Al Farsy (1984). *Qurani Takatifu*. Nairobi: The Islamic Foundation Publication. Chapa ya nne.

Steere, E. (1870). *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar*: London: Macmillan.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la pili). Nairobi: Oxford University Press.

United Bible Societies (1952). *Bibilia*. Nairobi: Scripture Union.

Vutagwa, L. F. (2013). *Sifa za Kiuhalisiajabu na Umuhimu wake katika Utenzi wa Fatuma.* (1940 ) wa M.K. Dammann. Tasnifu ya M.A Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Wafula, R.M (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wales, K. (2001). A *Dictionary of Stylistics: Toleo* la Pili. Harlow: Pearson Education.

Walibora, K. (2010). *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* 17(2010): 143-157.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi Msingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha fasihi: Similizi na Andishi.* Nairobi: Focus Books.

Wamitila, K. W. (2004). *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi nyingine.* Nairobi: focus publishers.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi za fasihi. Misigi ya uchanganuzi wa fasihi*: Nairobi. Vide muwa Publishers.

Wa Mutiso, K. "Epic and long poem : Ukawafi wa Miiraji." Nairobi Holly family Basillica, Nairobi. 5th, may.2016.lecture.

Warnes, C. (2006). Magical Realism and German Idealism. Modern Language Review 101/2:488-498.

William, F. (2003) *Internatinal Encyclopedia of Linguistícts* : Nairobi. Oxford University Press.

Zamora, P. L. na Faris, B.W. (1995). *Magical Realism Theory:* History Community, London: Duke University Press.

Http / google (2005). Al Islam.Org/Kiswahili Vitabu: Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu. Haijachapishwa.

Http / google (2013). The Classic Literary Hero, Mswada ambao haujachapishwa.